

MASWALI NA MAJIBU

 ...?...Nina furaha kuwa hapa tena usiku huu katika ibada ya Bwana wetu. Na sasa, ninapooni ninyi nyote mkiwa a furaha na kuimba hizi nyimbo za kale za ajabu, wote mmejazwa na Roho Mtakatifu na kadhalika, inatufanya tujisikie vizuri sana.

² Nasi tuna furaha sana kujaribu kuchukua muda mchache wa wakati tena usiku huu kujibu swali moja mawili. Sisi... mimi nilichukua wakati wenu mwingi asubuhi, lakini natumai mlipata baraka ni—nilizokuwa nikinena. Ni...Mwajua, tunayo mengi ya kuongea, sivyo? Nasi tuna mtu wa kunena habari Zake, huyo ni Bwana Yesu.

³ Ndugu Teddy, uki—ukiweza, baki tu juu hapa kwa muda mchache. Niliambiwa kulikuwa na mtoto mgojwa humu.

⁴ Na kabla sijaanza hili, tuna Ushirika, kwa hivyo tunataka—hatutaki kuchukua wakati mwingi sana—na labda ubatizo. Na kwa hivyo na—nataka ku—kuwaombea wale wote wanaotaka kuombewa kwanza...?...kuwaombea wagonjwa kwanza, kabla hatujaanza.

⁵ Na sasa, kama...Teddy, ukipenda, imba wimbo huu, Ni *Tabibu wa Karibu*. Nasi tutawaita wagonjwa na kuwaombea baraka hapa. Wangapi wamekuja kuombewa usiku huu? Kunao wengine hatukuwaombea asubuhi. Je, mnaweza kuinua mikono yenu...?...[Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]...na kusikia ushuhuda huo, na kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake wote. Mungu asifiwe ambaye toka kwake baraka zote zinatiririka. Sivyo?

⁶ Sasa, tutaanza upesi sana kwa shuhuda hizi sasa, nasi jaribu, kunradhi)—kwa maswali. Na natumai kuwa Mungu atamimina baraka zake hivi.

⁷ Na sasa, usiache nikayaendea kwa muda mrefu sana. Ndugu Cox ninawaonya, wewe na mashemasi mnaokaa kwenye mstari wa mbele mnisimamisha ninapo—inapofikia wakati wetu wa Ushirika (mwaona?) kwa sababu naliwakawisha sana. Nitajaribu kwenda upesi niwezavyo. Na ndipo, kama siyamalizi Jumapili hii, nitayaendea Jumapili ijayo, kwa hivyo.nitajaribu kuyamaliza usiku huu.

⁸ Ni maswali mazuri sana. Nami nawaambieni, marafiki, kama si mkutano wa ufufuo na kadhalika unaoendelea, ningependa kuchukua juma moja hivi katika mafundisho ya Biblia ya—ya Mwanzo, na Kutoka na Ufunuo, na kadhalika na—na kuwa tu na wakati m—mzuri kabisa. Napenda maswali ya kindani na mafundisho ya biblia, mradi tu hamwendi kando kwa

ubuni fulani. Kaeni tu moja kwa moja katika Neno la Mungu la kale, lililo dhahiri na lisilotiwa najisi; litakupitishieni. Je, hamwamini hayo? Vema.

⁹ Asubuhi hii tuna baadhi—baadhi ya maswali mazuri sana, mengine yayo kuhusu wale mia na arobaini na nne elfu, wao ni akina nani, na wangukuwa sehemu gani? Na-na kuhusu Bibi-arusi. Jamani, mambo mengi tu, na maswali ya kindani. Nami ninayo machache ambayo sikumaliza.

¹⁰ Sasa, usiku huu tutaanzia papa hapa kwa hili, na kumuuliza Bwana atusaidie. Na sasa, hatuwezi kufungua Biblia. Tunaweza kufungua kurasa zake. Lakini katika Kitabu cha Ufunuo, Yohana alipotazama naye akaona Mmoja ameketi juu ya kile Kitu cha Enzi, na kulikuwa na—Yeye alikuwa na Kitabu mkononi Mwake. Na hakukuwa na mtu aliyestahili kukitwaa Kitabu kile, wala kuifungua Mihuri, wala hata kukitazama. Hamna mtu Mbinguni, hamna mtu duniani, wala hakuna mtu chini ya nchi wala po pote aliye—aliyestahili. Naye akamwona Mwana-kondoo kama kwamba amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye akaja na kuchukua Kitabu kile toka mkononi Mwake na kufungua hizo Mihuri, ilikuwa ni Yesu Kristo.

¹¹ Sasa, nilikuwa nikiongea na mtu fulani asubuhi hii, mfanyi biashara mashuhuri sana mjini, aliyeniambia mimi kuhusu kwenda Afrika na India; yeye alisema, “Mbona, wamekwisha kumuua jemadari Mwingereza kule.”

Nilisema, “Hilo linanipasaje mimi?”

Yeye alisema, “Unarudi kule ambapo mauaji hayo yote yanaendelea, hizo ghazia nyingi, na mengineyo?”

Nilisema, “Hakika, huko ndiko ninakohitajika, kwa maana Bwana anitaka niende huko.”

Yeye alisema, “Na wakikuuja je?”

Nilisema, “Wema, Mungu akitaka nivawe, nitauawa tu, hivyo tu.”

Na yeye akasema, “Jamani!” kasema, “Ndugu Branham, haikupasi kuwaza hivyo. Vema,” kasema, “sijui. Nadhani wewe u wa kidini, nami nadhani u mtu mzuri,” yeye alisema, “lakini hata walimuua Yesu Kristo.”

Nilisema, “Hakika, yalikuwa mapenzi ya Mungu.”

Yeye akasema, “Ati nini? Mapenzi ya Mungu?” Mimi... Na mtu huyo amekuwa akienda kanisani (amekaribia umri wa miaka sabini), amekuwa akienda kanisani... Yeye alikuwa amekuzwa toka utotoni katika kanisa nzuri mjini humu, na amekuja—na hajajua kamwe kwamba yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa Yesu kufa.

¹² Naam, nilisema, “Ndugu, Yeye aliuawa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, tangu mwanzo. Yeye aliuawa kabla hata hajaja duniani.” Na huyo ni Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa tangu kuwekwa msingi ya dunia.

¹³ Hebu tunene Naye kwa muda mchache kwa ajili ya maswali haya. Sasa, Baba, hatustahili, na tumeshindwa, kufungua kile Kitabu au kukitazama. Lakini hebu na yule Mwana-Kondoo aje sasa usiku huu, Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, achukue vitu vilivyo vya Mungu na avitoe kwa kusanyiko hili. Na Roho Mtakatifu atwae maneno haya, na yasiwe maneno yangu wala maneno ya mwanadamu, bali na yawe Neno la Mungu kwa kila moyo wenye njaa. Kwa kuwa twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

La kwanza hapa (hatujayachanganyisha wala lo lote, lakini jinsi yalivyoletwa). Laonekana kuwa zuri sana. Kwanza, wangapi wanapenda maswali, hebu tuone . . . ? . . . Vema, hilo ni jema. Kwa kadiri nijuavyo tu.

15. Basi. Je, mtu anapokufa huenda Mbinguni au—au kuzimuni mara moja, au wao hungoja hukumu?

¹⁴ Hilo ni swali nzuri mno. Na lafanya—lilifikiriwa kwa makini, kwa sababu kila mtu ana hamu, yeye atakuwaje baada ya maisha haya kwisha? Kila mtu ana hamu. Vema sasa, mimi—nionavyo mimi, si—sijui. Yanipasa nijibu kwa Biblia.

¹⁵ Nadhani mwanamke fulani alipiga simu kwa dolla hamsini muda mchache uliopita toka Los Angeles, ya muda upatao dakika thelathini na tano au arobaini, au labda zaidi, ya mbali, akijaribu kunishawishi nisema kuwa ni halali na ni sawa kwake kuachana na mume wake na aolewe na mtu mwingine, singefanya hilo. La! Nilisema, “La, bwana!”

Yeye kasema, “Vema, mume wangu ni mwenye dhambi, na mtu huyu ni Mkristo.”

¹⁶ Nilisema, “Hilo si kitu kamwe. Utazini bila shaka.”

Kasema, “Vema, mimi nina ugonjwa wa kifua kikuu, na hakuna haja kwangu kuishi kama siwezi kuolewa na mtu huyu.”

¹⁷ Nilisema, “Vema umepumbazika tu na hujashikwa na mapenzi, sababu haiwezekani, hivyo tu, kwa sababu huyo ni mume wako. Na umetoa nadhiri uishi naye hata kifo kitakapowatenganisha. Kitu kingine cho chote mbali na hicho ni uzinzi.” Na kwa hivyo, yeye alizidi kusesitiza. Nikasema, “Bibi, hakuna haja . . .”

Yeye alisema, “Ukiniambia tu ni sahihi.”

Nilisema, “Siwezi kufanya hivyo.” Nilisema, “Nina . . .”

Akasema, “Vema, Ndugu Branham, tunakuamini sana.”

¹⁸ Nikasema, “Basi sikiza yale ninayojaribu kukwambia. Nakwambia Kweli, kwa maana siwezi kusema lo lote ila

alilosema Mungu.” Mungu alisema hiyo ni kweli, kwa hivyo ndivyo ilivyo hasa. Ona? Nilisema, Hivyo ndivyo hasa ipa—ipasavyo kuwa, na haina budi kuwa hivyo.”

¹⁹ Na sasa, katika maswali haya, hivyo ndivyo tuyatakavyo yawe. Sasa, imedhaniwa daima... Sasa, ndani humu, unatambua, katika hili kundi ndogo la watu usiku huu, huenda labda kuna mawazo mbali mbali, nasi twadhani yote ni mazuri, kila moja yayo. Wazo lako ni zuri, na ni... Lakini sasa, itupasavyo kufanya, yatupasa kuwa na mtu fulani... Kama tu bata bukini, bata, cho chote, kila kitu kina—nyuki—kila kitu kina kiongozi wake. Nyuki-malkia akifa, mwajua nini hutendeka. Kiongozi wa bata akifa, yawapasa kumchagua mwingine, Ha—hawana budi kuwa na kiongozi.

²⁰ Na mtu hana budi kuwa na kiongozi; na kiongozi ni Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu aweka Kanisani kwanza, mitume, baada ya hao, manabii, na kadhalika.

Mtu mmoja muda mchache uliopita, alisema, “Naam, Ndugu Branham, hatuhitaji mtu ye yote atufundishe. Roho Mtakatifu ajapo hatuhitaji mtu ye yote atufundishe.” Kasema, “Biblia yasema ham—hamhitaji kufundishwa.”

²¹ Nilisema, “Basi mbona roho Mtakatifu yule yule aliweka Kanisani waalimu?” Ona, ona? Yeye aliweka Kanisa katika utaratibu. Ndivyo ilivyo. Yatupasa kuwa na waalimu. Naam.

²² Lakini haikupasi uwe na ye yote... Haipasi akufundishe akikwambia, “Usizini; usiape, na chukua...” Wewe bila shaka umekwisha kujua hayo. Dhamiri yako ya Roho Mtakatifu hukwambia ni kosa kufanya hayo.

²³ Lakini kuhusu mafundisho ya Maandiko, yahitajika upako wa Roho Mtakatifu. Naam. Na Mungu ameweka Kanisa katika utaratibu kwa mitume na manabii na vipawa vya uponyaji na miujiza, na kadhalika. Yeye aliweka Kanisa katika utaratibu na kuweka waalimu na kadhalika ndani mle kuongoza na kusimamia Kanisa Lake. Na asubuhi hii, sisi—kama tulivyosema, Yesu yumo duniani katika Mwili Wake... Na mwili Wake uendavyo, ni kama tu kivuli kinavyoonekana duniani. Kinaambatana nao.

²⁴ Sasa, watu wengi... Wa—Adventisti wanaamini kuwa mtu anapokufa yeye huingia kaburini na kukaa kule, nafsi, mwili, na kadhalika, siku ya kiamaa. Na wao... Wanaita hilo “kulala kwa nafsi.” Vema, hilo ni sawa. Ni zuri mradi tu wamemwamini Yesu Kristo na wamezaliwa mara ya pili, hilo halitawadhuru. Lakini sasa, kulingana na Maandiko, mtu afapo, kama yeye ni Mkristo, kama yeye amezaliwa mara ya pili, amejazwa na Roho Mtakatifu, haitampasa kamwe kusimama katika hukumu apate kufa. Ona? Yeye aenda moja kwa moja katika uwepo wa Mungu. Naye hatahukumiwa kamwe, kwa sababu amekwisha... Ona?

25 Hainipasi kusimama kwa ajili ya yale Kristo aliyonifanyia. Sasa nilikuwa mwenye dhambi, lakini kuhukumiwa kwa Kristo...Ja-jambo lote ndilo hili katika maneno machache: Mungu alisema, “Siku utakayokula ya hayo, utakufa.” Hilo latosha.

26 Sasa, Mungu hana budi kutimiza Neno Lake. Yeye hawezi kufanya lingine ila kutimiza Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Mungu. Vema basi Yeye hawezi. Ndipo, Yeye... Umetengwa na Mungu. Ile... Ndiposa umezaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukinena uongo. Kwa hivyo unapozaliwa, asili yako ni mwenye dhambi. Kwa hivyo hakuna lo lote kamwe uwezalo kufanya juu yake. Singeliweza kufanya cho chote kujiokoa mwenyewe au wewe kujiokoa mwenyewe. Ni yale Kristo aliyotufanyia sisi katika Mungu—au yale Mungu alitufanyia katika Kristo. Ona? Si eti, vema, kama nawaza *hivi* au natenda *hivi*, ni kama Yeye alifanya *hayo*.

27 Vema sasa, sisi tuko ndani Yake. Ndipo Yeye alistahimili hukumu ya Mungu; Yeye alichukua hukumu ile. Naye hana hatia ya dhambi, hakutenda dhambi, bali alifanywa dhambi kwa ajili yetu. Kwa hivyo mradi tu umo katika Kristo, uko huru kwa hukumu. “Nionapo Damu, nitapita juu yenu.” Ona, Ona? Naam. Damu, ndiyo inayowaweka ninyi huru.

28 Sasa, mwenye dhambi ha...mwenye dhambi hana budi kusimama hukumuni. Na hakutakuwapo hukumu ila hii. Ni kama tu m-mviringo au upinde wa mvua wa Damu ya Yesu Kristo ikizunguka ulimwengu. Mradi tu umo ndani humu... kama Mungu angetazama duniani katika hali yake usiku huu kwa njia nyingine yo yote isipokuwa kwa Damu ya Kristo, Yeye angeuangamiza katika muda wa sekunde moja. Yeye angepaswa kufanya hivyo. Bila shaka angeuangamiza. Hapo ndipo hukumu inapokuja.

29 Sasa, kama—au mradi tu mwanadamu yuko humu duniani, haijalishi kama mtu yule ni mlevi, na mcheza kamari, na mwenye dhambi wakuogofya, rehema za Mungu bado zinamfanyia upatanisho. Na mwanamke, huenda akawa, vyo vyote awezavyo kuwa, kahaba ama cho chote kile, Damu ya Yesu Kristo ingali inamfanyia upatanisho. Lakini mara nafsi yake inapoondoka katika mwili huu naye aenda ng'ambo yake, amepita rehema na kuingia hukumuni. Mungu amekwisha kumhukumu. Amekwisha. Amekwisha kuhukumiwa. Amekwisha kuhukumiwa.

30 Unajihukumu mwenyewe kulingana na vile unavyochukua ule upatanisho wa Mungu kwa ajili ya dhambi zako. Ona? Jihukumu mwenyewe. Humwoni Yeye kama atosha kukusamehe wewe. Ona? Kama wadhani Yeye atakusamehe, ungama makosa yako, Naye atakusamehe.

³¹ Ndipo kwa Roho mmoja (tazama) sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja. Na kama vile mwili huo ulivyofufuliwa na Mungu, ulifufuka toka kwa wafu, ukahesabiwa haki, umeketi kwa mkono Wake wa kuume katika nguvu na mamlaka Mbinguni, kwa hivyo hao waliokufa katika Kristo wamo katika Kristo, na ni huru kwa hukumu, na watakuja katika huo ufufuo.

³² Sasa, lakini tukifa sasa—tukifa sasa, tunaenda moja kwa moja katika uwepo wa Mwenyezi Mungu katika mwili wa kimbinguni. Kama ningemkuta Ndugu Neville juu kule, sisi sote tukifa sasa, saa moja tangu sasa ningemkuta; ningesema, “Salama, Ndugu Neville,” niongee naye. Singesalimiana naye kwa mkono; yeye ako katika mwili wa kimbinguni. Ningeonea naye; yeye angeonekana tu alivyo pale. Ningeonekana kama nilivyo. Lakini sisi tungeonea sisi kwa sisi, lakini hatungegusana, kwa sababu hatuna tena zile hisi tano za kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Ona? Lakini sisi tungekuwa wa milele, nasi tungeonana. Tungeishi katika mazingara yaliyobarikiwa karibu na yale madhabahu ya Mungu. Hamjui Yohana aliona wale nafsi chini ya madhabahu zikilia “Hata lini, Bwana, hata lini” kurudi tena duniani wakavikwe?

³³ Ndipo, Yesu, aliye ndani yetu sasa kwa jinsi ya Roho Mtakatifu, wakati mwili Wake wa kimbinguni, Roho Mtakatifu, atakaporudi pamoja na ule mwili uliotukuzwa, tutatukuzwa pamoja naye na katika mfano Wake. Mwaona ninalo maanisha? Ndipo nitamwamkia kwa mkono na kusema, “Tumefika, Ndugu Neville.” Kisha tutakuwa . . .

³⁴ Tazama. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, walipokuwa na Ushirika wao, akasema, “Sitakunywa tena uzao wa mzabibu hata siku ile nitakapounywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu.” Sivyo? Ona? Naam, Kwa hivyo, sisi . . . Wafu wanapokufa . . . Mtu aliyehesabiwa haki, anaposimama katika uwepo wa Mungu, huingia katika uwepo Wake kama kiumbe asiye kufa na kuishi katika mazingara yaliyobarikiwa ya amani hadi siku ile ambayo—atakaporudi tena.

³⁵ Sasa, kulikuwa na wakati ambapo watu hawakuingia katika uwepo wa Mungu walipokufa, wale waliotakaswa. Hiyo ilikuwa katika Agano la Kale. Wao walienda katika mahali paitwapo Paradiso, nazo nafsi za wenye haki zilingojea humo katika Paradiso. Lakini Paradiso palikuwa mahali ambapo Mungu aliweka hizo nafsi katika nchi ya ndoto, hata Damu ya Yesu Kristo ilipomwagika; kwa maana damu ya mafahali na mbuzi haingeondoa dhambi, ilifunika tu dhambi. Lakini Damu ya Yesu huondoa dhambi.

³⁶ Mwatambua kuwa—Yeye alipokufa pale Kalvari . . . Na Yeye aliporudi, aliwafufua toka kaburini wale watakatifu waliokufa chini ya kule kutakaswa kwa damu ya mafahali, na mbuzi, na ndama. Nao wakaingia katika huo mji (lo!) na kuwatokea wengi.

Picha nzuri jinsi gani! Tamani, laiti tungeipaka rangi kwa muda mchache. Mtazame Yesu alipokufa.

³⁷ Hapa, kama nisemavyo mara nyingi, naamini, kanisani humu, kuna o—orodha hapa kama, ndani humu mnaishi viumbe vinavyokufa. Na kila mmoja yumo katika kusanyiko hili kubwa la hatia, la weusi na giza. Watu wanaokufa huishi ndani humu. Sasa, au wao huvutwa na ushawishi toka u—upande huu, au toka upande *ule*. Huwezi kuwa hapa kiumbe wa kiroho, mwenye dhambi au mtakatifu, bila kushawishiwa toka kuzimuni au toka mbinguni. Mwili wako wa kimbinguni unakungojuu juu hapa. Lakini kama u mwovu, na mnafiki, na mtu asiyejali, mwili wako wa kimbinguni uko chini hapa, haijalishi unawaza vipi uko kule juu; kwa sababu tunda uzaalo mbele ya watu lathibitisha unakotoka. Kwa hivyo uko hapa jinsi ulivyo mahali pengine. Maisha yako unayoishi hapa yanaonyesha tu urithi wako ulivyo uondokapo hapa. Je, wafahamu?

³⁸ Sisi hivi sasa tu (lo, ninapowaza hilo)—hivi sasa tumetukuzwa katika uwepo wa Mungu, tu waamini waliozaliwa mara ya pili. “Kwa maana nyumba ya maskani haya iliyo ya duniani hii ikiharibika, tuna mengine yanayongoja Utukufuni,” si mahali penginepo, ng’ambo kule tayari yakingoja sasa. Na miili hii ya dunia hii inaogua kuvikwa hiyo isiyokufa. Sivyo? Magonjwa, na kuugua, na maumivu, na huzuni, na kuvunjika moyo, na... Ee! Nitafurahi nyumba hii yenye masumbuko itakapofungwa, nanyi, je? Naam, bwana! Tunaweza kuenda Nyumbani. Naam.

³⁹ Hili...Tuna—ugua tupate kuvikwa, Roho anaogua. Ee, utazamapo na kuona maumivu haya yote yametuzunguka, mikusanyiko yote, uvundo, na dhambi, na maisha yanayokufa, na uongo, na kila kitu, nadhani, “Ee, Mungu, umebaki muda gani?”

⁴⁰ Hivi karibuni nitahubiri mahubiri yangu ya mwisho, nitaiweka Biblia chini hivi na kuenda Nyumbani. Ee, utakuwa wakati jinsi gani. Na maskani haya yakwishapo hapa, haitachukua hata sekunde moja kufikia yale kule ng’ambo; hata nawe pia. Jamani! Si ajabu walisema:

Hili vazi la mwili nitalitupa nifufuke,
Na kunyakua tuzo la milele;
Na kupiga shangwe nitakapokuwa nikipitia
hewani... (Naam nikielekea juu)

⁴¹ Sasa, huko ni wapi? Tutaupata lini? Sasa! “Wale aliowahesabia haki, hao pia aliwatukuza.” Na, je, mnajua ya kwamba miili yetu iliyotukuzwa na isiyokufa inatungojuu katika uwepo wa Yesu Kristo sasa hivi, inatungojuu sisi tuje?

⁴² Je, mwajua mtoto mchanga azaliwapo duniani humu, kabla hajazaliwa yuna uzima. Lakini hajazaliwa bado. Na mara tu mtoto huyo ajapo a—a—anapoanza ku—kuzaliwa... Mapafu

yake yamefungamana, ni maiti. Misuli yake inatetemeka-tetemeka na kutikisika-tikisaka. Lakini jambo la kwanza, kugongwa tu kidogo kumoja kuwili hivyo [Ndugu Branham aonyesha—Mh.], na ata-[Ndugu Branham anakokota pumzi—Mh.] pata pumzi yake. Kuna nini? Mara tu huo mwili wa kawaida uanzapo kuumbika katika mama, kuna mwili wa kiroho unaongoja kumpokea mara tu huyo mtoto mchanga azaliwapo.

⁴³ Na bila shaka kama vile kuna mwili huu wa kiroho unaozaliwa, kuna mwili wa kawaida unaongoja kuupokea mara tu u—unapoondoka ulimwenguni humu. Ona? Na kadhalika, kurudi tena Edeni (ona?), kurudi moja kwa moja.

⁴⁴ Sasa ndani mle, Mungu... Naam, mauti, hilo tu—hilo linatupilia mbali uchungu wote wa mauti uliopo. Na si ajabu Paulo angesimama na kusema, “U wapi, Ewe Mauti, uchungu wako? Ku wapi Ewe kaburi kushinda kwako?” Yeye alisema, “Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Naam, marafiki! Nyumba ya maskani haya iliyo ya duniani ikiharibika tayari tunayo mengine yanayongoja, kwa hivyo sahau hayo.

⁴⁵ Sasa kwako, rafiki, kama wewe uliyeuliza hili ni mwenye dhambi, Mungu akurehemu. Naam, bwana! Hauko tu chini ya hukumu sasa, si hapa, la! Utafanikiwa na kuendelea. Na hayo yote ni kwa rehema za Mungu. Hayo yote ni kwa rehema za Mungu kwamba ufanikiwe na kufanya ufanyayo. Hilo ni kweli. Lakini hivi karibuni, kama wewe u mwenye dhambi na nafsi yako iponyoke, itaingia hukumuni na itahukumiwa. Ndiposa, utatupiliwa mbali, na utakuwa katika mateso hata utakaporudishwa duniani humu tena. Na utapokea mwili usiokufa, mwili usiokufa ambao hauwezi kufa, na utatupiliwa mbali katika giza la nje ambapo kutakuwa na kilio, kuomboleza, na kusaga meno. Utatupwa kuzimuni, ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki, na utateswa katika nyakati zote zijazo. Yesu alisema hayo. Hiyo ni picha nyeusi, lakini ndivyo Biblia isemavyo.

⁴⁶ Kama Mungu alihukumu dhambi hivyo na iligharimu gharama kuu kama hiyo, itakuwaje kama roho hao wachafu wataachiliwa tena? Tungekuwa na jambo lingine kama tumekwisha kuwa nalo katika miaka elfu sita iliyopita. Sivyo? Hakutakuwa na nafasi tena.

⁴⁷ Sasa unasema, “Vema, naamini kuwa unapoingia kaburini u—unaenda kuzimuni.” Mwili wako unaenda kuzimuni, naam. *Kuzimu* maana yake ni “utengano.” Mauti maana yake ni “utengano.” Mwili wako unakufa, unatenganishwa. Unatengana na wapendwa wako hapa, lakini hayo siyo tunayonena. “Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.” Ona?

48 Sasa, unapo—kama itakupasa kusimama hukumuni mwa Mungu, utahukumiwa na Mungu mwenye hasira. Na Mungu yuaenda—amekwisha kutangaza yale Yeye atakayofanya. Kwa hivyo unajua hukumu yako itakavyokuwa kabla hata hujafika kule. Kwa hivyo jambo la kutenda ni kuokolewa na uwe na huu mwili uliotukuzwa. . .

49 Tazama. Kama yanipasa—kama roho yangu. . . Tazama, sisi si kitu kilichokufa; sisi tu hai. Kama—kama—kama dawati hili hapa—kama ubao huu ungekuwa na uhai ndani yake uliomo katika kidole changu, hayo mauti—na ubongo wa kuusogeza, ungeweza kusonga kama kidole changu kisingavyo. Hatujaumbwa kwa kitu kama hicho. Sisi tumeumbwa kwa—kwa—kwa chembechembe hai, na za uhai, na nyuzi-nyuzi; na kuna roho humu anayeuongoza wote. Hebu katazame inavyojimundu haraka; mkono wangu unagusa hicho. Naam, mara. . . Hapana budi pawe na urejeo halisi na usio halisi. Mara tu baada ya kidole changu kugusa hicho, kinahisi hayo. Hilo linaingia mawazoni upesi, na mawazo yangu yasema, “Hicho ni baridi.” Inarudi tena. Mwaona hilo lilivyo jepesi? Jepesi kuliko wazo, tendo hilo hapo ni jepesi kuliko cho chote kile. Ni nini? Kuna kitu fulani hai ndani mle, na hiyo neva inaipasha habiri akili, mwaona ninalomaanisha? Neva inaigusa, inahisi, na inaambia mawazo, “Ni baridi.” Nia inasema ni baridi, kwa sababu neva imeihisi. Jamani! Nena kuhusu mapambo.

50 Ndiposa—yote hayo. . . Jinsi Mungu ajuavyo upesi sana kila wazo tunalowaza. Kila kitu tunachofanya, Yeye akijua.

Kwa hivyo mwamini anapokufa, yeye huenda katika uwepo wa Muumba Wake, Mungu wake. Na mwenye dhambi, anapokufa, yeye huenda kwa kituo chake. Ndipo katika kule kurudi. . . Sasa, naongea sasa kuhusu walio wateule.

51 Lakini kuna wengine watakaofufuka katika ufufuo wa pili, ambao watasimama hukumuni na mwenye dhambi, wahukumiwe pamoja naye. Nataka nihakikishe mnafahamu hilo. Ona?

52 Sasa, kutakuwa na. . . 1a kwanza litakalotukia ni ku—kuja kwa Bibi-arusi. Kutakuwa na watu ulimwenguni. . . Mimi. . . Huenda ukatofautiana na hili kidogo, lakini sikiza kwa makini. Kwa sababu tu kwamba ulimpokea Yesu kama Mwokozi wako binafsi, hilo si kusema kuwa utanyakuliwa. Huko ni kwa wale walio Wateule, watakaonyakuliwa. Kutakuwa na masalio watakaoachwa duniani watakaopitia katika yale mateso na ile dhiki iliyo kuu. Kanisa litatwaliwa kwa kunyakuliwa.

53 Je, ni wanawake wangapi humu ambao hawajui kuwa unapotaka kuikata jora unaitandaza hivi, na kuweka bombwe lako juu yake hivi, na unakata kitambaa kile kulingana tu na ile bombwe. Sivyo? Na kitambaa kile kilichobakia ni cha aina iyo hiyo iliyoko kwenye ile bombwe. Sivyo? Lakini ukachukua hiki.

Waweza kuweka hicho kando kwa matumizi ya baadaye, lakini kitambaa kile—ulikokitoa . . .

⁵⁴ Sasa, nani awekaye bombwe? Mungu, kwa uchaguzi. Amina! Mungu! kwa uteuzi huweka bombwe lile. Yeye alisema, “Sasa, nimechagua tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu . . . Nikaweka hawa . . .” Mbona, Yesu aliwaambia wanafunzi kuwa Yeye alikuwa pamoja nao, na aliwachagua, na kuwajua tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Sivyo? Kwa hivyo Mungu huweka lile bombwe. Sasa, kutakuwako walio Wateule watakaonyakuliwa. Na kutakuwa na kundi la watu walio wazuri, wanyofu, wanaoishi kitakatifu, watu waliookolewa na Mungu, ambao hawatanyakuliwa; nao watafufuka katika ufufuo wa pili, kwa sababu . . .

⁵⁵ Ee, na—natumai hamtanikasirikia mimi nikifanya jambo fulani dhahiri sana hapa kwenu. Ona? Msifanye hilo. Ya—yanipasa nilisema, kwa sababu li—linanisonga mara kwa mara (mwaona?) kulisema. Tazama. Sasa tazama. Basi nitasema hili: kuna watu wanaoamini katika kuhesabiwa haki kwa imani (ona?), nao wanaishi maisha mema, masafi, na matakatifu; wanaamini katika kutakaswa pia. Narudia . . .

⁵⁶ Mtazame Yuda Iskariote. Yuda iskariote aliheesabiwa haki alipomwamini Bwana Yesu Kristo na kumkubali Yeye kama Mwokozi wake binafsi—Yuda Iskariote. Yuda Iskariote aliisha takaswa katika Yohana 17:17 na akapewa nguvu katika Mathayo 10 aenda na akatoe pepo. Na Yuda Iskariote alirudi, akiisha kuponya wagonjwa na kutoa pepo, akarudi amefurahi na kupiga shangwe kwa kadiri mtakatifu anayejigaragaza ye yote mliyewahi kumwona awezavyo. Sivyo? Biblia ilisema hivyo. Lakini alipofikia Pentekoste, yeye alionyesha alivyo hasa. Sasa tazama hilo—roho huyo.

⁵⁷ Kuna watu ulimwenguni siku hizi, Wakristo wazuri wanaoamini kuhesabiwa haki, wengi wao, maelfu, mamilioni wanaamini kuhesabiwa haki. Lakini hawataki kamwe kutakaswa. Tunesema hao ni Wapresbiteria, Wa-Episcopalia, na wengineo. Wanaamini kuhesabiwa haki; wanakuhubiri. Na ni vizuri; wako sahihi.

⁵⁸ Lakini sasa, wale—wale Wanazarini, Wa-Pilgrim Holiness, Wamethodisti Huru walisonga mbele wakashiriki katika kutakaswa. Wanaamini kutakaswa. Sawa! Wako sahihi. Nao hupata ushindi, na kupiga shangwe, na kumsifu Bwana. Wako sahihi, wako sawa. Lakini mwambie ye yote kati yao kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, na nguvu zile, na ishara, na maajabu, wataonyesha sura yao papo hapo. Kasema, “Sitaki hayo kamwe. Siamini . . .” Vema, hata watu wangu Wanazarini wazuri, wanaamini kuwa mtu akinena kwa lugha yeye ni wa ibilisi. Vema, ndugu, mnafanya hivyo, ninyi . . .

⁵⁹ Naam, walimfukuza Dk. Reedhead toka kwa Sudan Missions, aliyekuwa rais wao, kwa sababu yeye alinena kwa lugha. Kasema, “Hatumtaki.”

⁶⁰ Nilisema, “Hamwezi kuhubiri kama Paulo basi. Hamwezi kukubali Injili ya Paulo, maana Paulo alisema, “Msizuie kunena kwa lugha.” Naam. Lakini wao—wao wanasema ni kwa shetani. Wameona maigo mengi, na kuyabeba yote pale. Ona? Lakini hilo ni kanisa lililohesabiwa haki na kutakaswa; lakini wanakataa kuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kazi tofauti na utakaso. Lakini ni—ni kazi tofauti. Bila shaka ni tofauti.

⁶¹ Kuna vitu vitatu vilivyotoka katika mwili wa Kristo. Na vitu vivyo hivyo vilivyotoka mwilini Mwake ndivyo tunavyotumia kuingia katika Mwili Wake. Kulikuwa na maji (sivyo?), Damu (sivyo?), na Roho. Na—Yesu—na Maandiko yalisema, “Kunao watatu washuhudia Mbinguni, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hawa watatu ni Mmoja; hawa ni Mmoja. Lakini kuna watatu washuhudia duniani; wao si Mmoja,” yeye alisema, “Hao hupatana kwa habari moja; Maji, Damu, na Roho.” Sivyo?

⁶² Sasa, huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana. Huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu—lakini unaweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa. Na unaweza kuhesabiwa haki na kutakaswa pia na usiwe na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ona? Hiyo ni kweli. Hayo ni Maandiko. “Hawa watatu,” yeye alisema, “wanashuhudia duniani, maji, Damu, na Roho; navyo vyapatana katika habari moja.” Ona? Si mmoja, lakini wanapatana katika habari moja.” Ona? Si mmoja, bali vinapatana katika habari moja, kwa sababu ni Roho yule yule kwa kipimo. Mungu hutupa Roho kwa kipimo.

⁶³ Sasa, Luther, chini ya kuhesabiwa haki, hayo ndiyo yeye aliyohubiri, Sivyo? Luther alihubiri, “Wenye haki wataishi kwa imani.” Yeye alikuwa na ujumbe mkuu. Na hiyo ilikuwa sehemu ya Roho Mtakatifu. Ndipo Luther, ujumbe ulipotangazwa—Mungu alikuwa yuaenda kuinua Kanisa Lake na alitume nje likiwa kuu zaidi (jamani!) Luther alisema, “Ee, tunaamini tumeipata katika Neno.”

⁶⁴ Lakini John Wesley akasema, “Ee, la!” Yeye na George Whitefield pamoja nao, walisema, “Tunaamini katika utakaso—huo ni—ya kuwa ni kazi halisi ya pili ya neema.” Sivyo? Nao walihubiri Damu. Vema, kama Luther hakutaka kusonga mbele, Mungu aliitoa tu kwa Methodisti ya Ki-Wesley. Ona? Nao wakaipata. Ndiposa wakawa na ufufuo ulioenea ulimwenguni kote.

⁶⁵ Na Kanisa halisi... Vema sasa, wakati huo ujapo... Sasa, ndipo ukaja ushuhuda wa Roho Mtakatifu wa ishara na maajabu, na miujiza. Sasa, Wesley hataki kukubaliana nao sasa, kama Wesley angalikuwa duniani na Martin Luther awe duniani nyakati hizi, wangelikubaliana nao, lakini walipata

tu zamu ya pili ya—ya—ya nne au ya tano ya mitume, nao wakautangaza kote.

⁶⁶ Sasa, Pentekoste walipokea na kuamini katika kunena katika lugha. Kisha wakakugeuza kuwa ndiko “ishara mathubuti,” hata ikampasa kila mtu anene kwa lugha. Hilo ni kosa. Lakini sasa—sasa walirudi... Hizo zilikuwa dalili zilizotolewa na Mungu. Kama tu vile nisivyoweza kujizuia, kwa sababu nina macho ya samawati, au... Mungu alinipa tu hayo. Hiyo ni karama Yake Kanisani. Mungu aliziweka humo, “Mungu ameweka Kanisani...” Ona?

⁶⁷ Sasa. Lakini walipokuja nao... Sasa, walikuwa na baraka kuu, walienda mbele zaidi ya Walutheri au Methodisti, wote hao. Na sasa, wamejiundia dhehebu hata wao ni wabaya zaidi kuliko Methodisti na kadhalika—Wapentekoste. Ndiposa, wamefikia mahali ambapo zamu ya pili na ya tatu... Imekuwa miaka arobaini na nne tangu walipoanza kunena kwa lugha. Lakini huu mti wa Mungu una matunda tisa mbalimbali juu yake. Sasa, waweza kupata yote ya matunda haya. Ona? Mungu ameyatuma hayo, lakini yote pamoja yatoka kwenye mti ule.

Sasa, kuhesabiwa haki, kutazame.

⁶⁸ Tazama ujumbe wa asubuhi ya leo. Hukumu ilipowekwa, na vitabu vile vikafunuliwa... Sasa, Yesu yuaja na kumi elfu mara kumi elfu ya watakatifu, ndiposa hukumu ikawekwa. Hapa wao wote kwenye ile hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi (kama tulivyosoma Maandikoni), na Vitabu vilifunguliwa; na Kitabu kingine kilifunguliwa ambacho kilikuwa kile Kitabu cha Uzima. Na hawa walionyakuliwa walikuwa wakiwahukumu. Sivyo? Wale walioenda nyumbani na kupokea miili yao iliyotukuzwa, na kuishi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, walikuwa hapa katika ile Hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi, wakiwahukumu hao. Yeye alisema atabagua kondoo na mbuzi.

Sasa, mnasema hapa, “Naam, tazama sasa.” Unasema, “Hiyo itakuwa... Wapi, Ndugu Branham?” Katika ile Hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi.

⁶⁹ “Na kule kunyakuliwa je?” Vema, wakati wa kunyakuliwa... Yesu alifundisha hayo kama mfano. Naye aliyafundisha katika njia nyingi sana. Hapa kuna njia moja. Yeye alisema kuwa kulikuwa na wanawali kumi walioenda kumlaki Bwana. Na wakaona... Hao wote walikuwa wanawali, lakini wengine walikuwa na Mafuta katika taa zao na wengine wakamaliza Mafuta. Sivyo? Na wakati Bibi-arusi... Sasa, *Mafuta* yalikuwa nini? Hayo Mafuta yalikuwa Roho Mtakatifu; Biblia ilisema hivyo. Sasa tazama. Wao walikuwa wanawali. Sasa, nini maana ya *wanawali*? “Watakatifu, wasafi, waliotengwa, waliotakaswa.” Sivyo?

⁷⁰ Ningalikuwa na bilauri hapa ningewaonyesheni ninyi nini... Hapa, kwa mfano kama chupa hii hapa, kama ilikuwa

tupu, nami niliichukua, na ilikuwa chafu kupindukia. . . Nataka kuitumia. Vema sasa, jambo la kwanza nitakalofanya ni kuihesabia haki. Niichukue kwa sababu nataka kuitumia. Ni chafu, niliipata katika—katika zizi la nguruwe, au kokote kule. Sasa, kama mimi ni mtu kweli kweli, vema, sitaki kuweka kitu kisafi ndani mle ninachopaswa kutumia. Ni—ninapaswa kutayarisha kitu hicho kwanza. Sasa, jambo bora kufanya ni kuisugua, kuisafisha, na kuitakasa, sivyo? Sasa, nini maana ya neno *takasa*?—“Kilichosafishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi.” Viombo vya lile hekalu la kale vilisafishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi.

⁷¹ Sasa, kuna Kanisa: Mungu aliwachukua katika wakati wa Luther, kuhesabiwa haki; wakati wa Wesley, Yeye aliwatakasa; na katika wakati huu Yeye huwajaza. Ona? Yeye huweka Uzima ndani yao. Na wakati huu, Uzima Wake katika Roho Mtakatifu. . . Roho Mtakatifu akawachukua; Roho Mtakatifu akawatakasa; Roho Mtakatifu akawajaza. Ona? Yote ni Kanisa lile lile.

Lakini sasa tazama. Sasa siku hizi. . .

⁷² Sasa, nadhani kuwa Luther, Wesley, na wale wote, wengine wote, wengi wao watanyakuliwa. Walikuwa na sehemu ya Roho waliyohubiriwa; wakaamini.

⁷³ Sasa, katika kule kunyakuliwa. . . Kuna watu siku hizi walioenda katika madhehebu hayo ambao hawakusonga mbele. Ni. . . Kuna dhehebu moja tu, hilo ni Kanisa la Mungu; na limesonga mbele haidhuru. Lakini madhehebu haya yalivunja mambo haya hivyo. Na watu wengi siku hizi watatazama ubatizo wa Roho Mtakatifu na kusema ni upuzi. Lakini hata hivyo wamehesabiwa haki; bali hata hivyo wametakaswa. Lakini wao husema “Ee, huko ni kukosa adabu, upuzi huo.”

⁷⁴ Najua ibilisi ameweka kila namna vitisho vya bandia. Hapo ndipo unapopata matofaa mazuri, ni karibu na mahali ilipo ile sanama ya kutisha ndege. Naam. Nenda tu nyuma ya kitu hicho, endelea kula matofaa. Ona?

⁷⁵ Sasa, hili. . . Ndipo Mungu akajaza kwa Roho Mtakatifu. . . Kisha akaweka Kanisa Lake nje alitukuze. Katika kule kuja kwa pili, ndilo hili Kanisa linarudi, Bibi-arusi. Sasa tazama. Ona kama wao wanapitia katika ule wakati wa ile dhiki iliyo kuu. Yeye alisema, “Hawa wanawali, walikuja na kusema, “Tupeni Mafuta yenu kidogo.”

“Hayo, Bwana arusi yuaja!” Sauti ikapazwa, “Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki.”

Na hawa wanawali, ambao ni wanawali, watakatifu, waliotakaswa (waza hilo), watakatifu, watu waliotakaswa wasio na ubatizo wa Roho Mtakatifu, wao walisema, “Tupeni Mafuta!”

⁷⁶ Na Kanisa lilisema, “Tunayo tu ya kututosha sisi. Nendeni mkaombe mkisihi sana.” Lakini kumechelewa sana wakati huo. Kwa hivyo, kanisa likaingia Arusini, na hawa wengine wakatupwa katika giza la nje (sivyo?), ambapo kulikuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno; nao wakapitia katika mateso, wakaugua, wakafa.

⁷⁷ Yesu alirudi tena duniani. Ule Utawala wa Miaka Elfu ukaanza, miaka elfu pamoja Naye. Wakaja wale we—wenye haki na wasio haki. Nao walimhukumu kila mtu. Na mbuzi zilikuwa upande mmoja na kondoo upande mwingine. Ndiposa Mungu alikuja na kutwaa Kanisa toka mapana ya dunia kwa ajili ya mkutano wa kambi, ambapo sisi sote tutakusanyika pamoja na wapendwa wetu. Ona? Tofauti yake ndiyo hiyo.

⁷⁸ Sasa, watu hawa hapa . . . Bila shaka tunapokufa, kama tuko katika Kristo Yesu tunaenda juu kuwa na huo Mwili mkuu kule ng’ambo, ikiwa tumo katika Yesu Kristo. Kama sisi tu wenye dhambi, tunaenda kuwa na kundi kuu la wasioamini; na Mungu alisema sehemu yetu ilikuwa pamoja na wanafiki, na wengineo, kuzimuni. Amina! Huenda isiwe dhahiri sana.

Lakini, hebu tuone sasa kama tukiweza kupata . . . Kijikaratasi, kidogo hapa.

16. Tafadhali fafania Kutoka sura ya 24 sura ya 4 na kifungu cha 24. Maandiko haya yamaanisha nini—kuwa Mungu alikusudia kumwua Musa au mwanawe? Na ni kwa nini?

⁷⁹ Twajua haya yaliko, Kutoka 4:24. Hilo ni swali nzuri. Sasa, hapa tutayasoma—papa hapa kwa muda mchache. Kutoka 4:24:

Ilikuwa walipokuwa njiani mahali pa kulala BWANA akakutana naye akataka kumwua.

Wangapi wanakumbuka hadithi hiyo? Naam, Mungu alimpa Ibrahimu, vizazi vingi kabla ya siku za Musa, ile ishara ya tohara. Na hiyo ni agano alilolifanya Mungu, ambapo kila Myahudi anapaswa kutahiriwa. Sivyo? Kila mtu apaswa . . . Hiyo ndiyo ishara.

⁸⁰ Nasi je, tumetahiriwa siku hizi? Kwa Roho Mtakatifu, si katika mwili.

⁸¹ Sasa. Sasa, Mungu alitoa maagizo haya, “Na kila mwanamume hana budi kutahiriwa.” Kisha Mungu, alipomwita Musa aende chini kule na kuwakomboa wana wa Israeli, Musa hakuwa amemfanyia mwanawe hiyo ishara ya ukombozi. Mwaona lile ninalomaanisha?

⁸² Ni kama mimi nikisema, “Ninyi kanisa letu sasa, kila mmoja wenu—aingie na kubatizwa hapa kwa maji, nasi tunawaweka ninyi kwenye orodha ya kanisa. Sisi sote tunaenda utukufuni pamoja.” Naam, ndugu, hayo si Maandiko. Isipokuwa umezaliwa mara ya pili, umetahiriwa kwa Roho Mtakatifu . . . Yakupasa kuwa hivyo. Sijali wewe u mzuri jinsi gani, u wa kanisa gani,

wazazi wako nao walikuwa wazuri vipi, isipokuwa wewe kama mtu binafsi umezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, hutanyakuliwa kamwe. Ona? Huwezi kwenda. Hii ndiyo ishara ya ukombozi, ile tohara; na tohara; na tohara ni kwa Roho Mtakatifu. Sasa Mungu. . .

⁸³ Yule—yule muuliza aliuliza hivi: “Je,—je Andiko hili lakusudia kuwa Mungu alinuia kumwua Musa au mwanawe? Na ni kwa nini? Mungu alitaka kumwua Musa?” Na Sipora ndiye pekee aliyemwoko pale. Maana Sipora alishika jiwe gumu, akaondoka, akaenda na kuikata govi ya zunga la mwanawe, na kuibwaga mbele ya Musa na kusema, “Hakika wewe u bwana arusi wa damu kwangu mimi.” Sivyoy?

⁸⁴ Na Mungu angalichukua uhai wa Musa, lakini labda Malaika alikuwa amesimama pale, “Sipora! Lishike upesi!” Ona?

⁸⁵ Na Sipora akaenda na kumtahiri mtoto yule. Kasema, “Musa una—unashughulikia sana mambo mengine yote na kuhusu safari yako, hata mwanako hajatahiriwa.”

Nashangaa mara nyingi kama . . . Wakati mwingine nimekutana na watu waliosema, “Ee, Mungu atukuzwe. Bwana anitaka nifanye kitu *fulani*. Yeye anitaka niende Afrika, niende India.”

⁸⁶ Nilisema, “Umewahi kumuuliza mtembeza maziwa ya kuuza kama yeye ameokolewa? Je, umewahi kumuuliza muuza magazeti kama amezaliwa mara ya pili? Na jirani yako je, wameokoka?” Ona? Naam, swali ndilo hilo. Ona? Kama unataka kwa moyo mwako. . .

⁸⁷ Hapa wakati fulani uliopita mwanamke fulani alikutana nami chini hapa—Florida. Na maskini mwanamke huyo, sina njia . . . Mimi si hakimu. Lakini kulikuwako na maskini mhubiri mmoja ambaye aliisha kuwa hapa na kuhubiri kwenye jukwaa hili. Na maskini mtu huyo katika nchi nyingine alikuwa ameo na ana mke, na watoto watatu wanne. Na mwanamke huyu alikuwa mjane. Nao walikuwa wametoka kule Texas, wakaja pamoja hapa katika motokaa kubwa ya Cadillac. Na mwanamke huyo akaingia. Naye ana haki ya kuvalia vyo vyote apendavyo, haijalishi kwangu; lakini kama mwanamke Mkristo yeye hakuvalia vile. Yeye alikuwa (Jamani!)—yeye alikuwa—alikuwa na pete kubwa na ndefu—hizo pete za masikioni (vyo vyote uziitavyo) zikining’inia chini hivi, naye alikuwa na taka nyi—nyingi kwenye mdomo wake; na—naye—na nyushi zimenyolewa naye alikuwa na nyushi zingine, zimechorwa kwa penseli. Kisha akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “Bwana ananiita mimi katika nchi za ng’ambo.”

Nilisema, “Anakuita?”

“Naam!” Naye alisema, “Naenda kule pamoja na mtu huyu.”

Nilisema, “Vema, kama Bwana anakuita, vema, vema.”
(Lakini kwa matunda yao...Haikuonekana kwangu kama... Ona?)

Kisha akasema, “Je, huamini Bwana...”

⁸⁸ Nilisema “Usiniulize. Kama Bwana ameisha kuambia fanya yale Bwana amekuambia utende. Lakini kwangu mimi, siamini hivyo, kwangu mimi. Nataka kukwambia wazi-wazi.”

Yeye alisema, “Vema, mbona wawaza hivyo?”

Nikasema, “Jambo la kwanza, kwa kuwa wewe u mwanamke uliyeolewa, haionekani vema kuwa na mwanamume huyu aliyeo, mnavyokaa chini hapa mjini pamoja. Kama mna kitu kinacholeta fedheha, ni hicho. Ona?” Nilisema, “Sasa, jambo la kwanza...”

⁸⁹ Nashangaa nini kingetendeka kwa mwanamke huyo? Jambo lile lile lingepa...Yeye ameendelea kujichafua hapa na pale bila kumpokea Roho Mtakatifu, kama tu mwanamke yule kule leo aliyenipigia simu akitaka kuolewa na mwanamume huyo, na kumwacha mumewe, akaolewe na huyo mwanamume, Yeye alikuwa amefikia mahali ambapo, labda wakati mmoja aliishakutana na Mungu, lakini alikuwa na tamaa mbovu ya kutamani vitu vya ulimwengu. Nami nilimwuliza; nilisema, “Je, umempokea Roho Mtakatifu?”

Yeye alisema, “Bado, lakini ninamtafuta.”

⁹⁰ Nilisema, “Mpokee Roho Mtakatifu kwanza, kisha atakwambia mume utakayekuwa naye.” Naam. Ona?

U—una...Ndivyoy ilivyo. Usipofanya hivyo, utakufa kiroho. Mungu ananena sana usiku huu. Lakini Yeye amekwisha kubisha moyoni mwako [Ndugu Branham agonga mimbara—Mh.] mara nyingi sana. Na hivi karibuni Yeye ataufunga mlango, na—na rehema imekwisha. Ona?

⁹¹ Bila shaka, Mungu angetwaa maisha yake. Yeye alisema alitaka kumwua. Sikiza jinsi Andiko lisomekavyo: kumwua. Sikiza yasemavyo Maandiko:

Ilikuwa walipokuwa njiani mahali pa kulala, BWANA akakutana naye akataka kumwua. (Musa. Sasa, tazama.)

Ndipo Sipora akashika—jiwe gumu na kuikata govi ya zunga la mwanawe, na kuibwaga miguuni pake, akasema, Hakika wewe u bwana arusi wa damu kwangu mimi.

⁹² Naam. Sasa, Mungu hakuwa akitaka kumuua huyo mwana. Mungu...Maskini mtoto huyo mchanga hakujuu la kutenda, hakuwa na hatia. Lakini jambo ni kwamba, ni baba wa mwana mchanga yule, aliyekuwa akishuka kwenda na huyo mtoto mchanga kuwakomboa wana wa Israeli chini ya ishara ya tohara:

huku mwanawe hata hajatahiriwa bado. Ona? Na Sipora aliikata kwa jiwe gumu, ile govi ya zunga, na kuibwaga chini, na kusema, “Wewe u bwana arusi wa damu kwangu mimi.”

17. Tafadhali eleza maana ya Andiko hili, na litatimia lini: Isaya 4 na 1. Asante.

Vema. Tatalifungua sasa hivi. . . Ninyi watu mlio na Biblia zenu na mnataka kufanya hivyo, tutaona jinsi. . . Sikupata nafasi kulitafuta hili, lakini nilidhani labda tutapata jawabu haidhuru. Ndilo hii.

Na siku. . . (Ee naam!) Na itakuwa. . . Na siku hiyo wanawake saba watamshika mtu mmoja wakisema, tutakula chakula chetu, na kuvaa nguo zetu wenyewe, lakini tuitwe tu kwa jina lako; utuondolee aibu yetu.

⁹³ Vema, ndugu sasa imekaribia sana kuwa hivyo. Ni kuanguka jinsi gani kumetokea nchini mwetu! Hebu niseme hili rafiki yangu Mkristo mpendwa. Hebu niseme hili kwa heshima itokayo kwa Mungu kwa kila mmoja; kama kulikuwa na. . . Nanyi watu hapa ambao mmesoma historia, tuko kwa njia hiyo ambayo kila taifa nzuri nyakati zote limeangukia, utovu wa uadilifu, kurudi nyuma moja kwa moja.

⁹⁴ Kama nilivyosema asubuhi hii. . . Kunradhi kwa kulirudia. Katika nchi za kigeni watu hunijia na kusema, “Ndugu Branham, mna wanawake namna gani pale? Vema, nyimbo zote ziimbwazo, nyimbo chafu za kale kuhusu wanawake wenu.” Naam. Wote huimba upunzi fulani kwa—kwa—kwa. . .

⁹⁵ Vema, mwajuaje? Je, mwataka niwaambieni katika maneno machache? Nitawaambia hakika. Ulimwenyu umo katika hali kama hii, kwa sababu ni Sodom na Gomora ya kisasa. Bila shaka! Kule California nilichukua gazeti. Nasahau ni maelfu mangapi kila mwaka wanaowashika, kujua, kuhusu ongezeko la walawiti. Hata tamaa zao za maumbile za—za—kati ya mume na mke, na kadhalika, zimewaondoka watu. Ni yale yale hasa Mungu alisema yangetimia. Na. . .

⁹⁶ Uwachukue baadhi. . . Ona nani anayependwa zaidi. Sikiza redio zenu, au televisheni, au cho chote mlichu nacho, mtaona. Ni jambo baya mno na chafu. . . Kuna nyimbo fulani kuhusu baadhi ya wanawake au kitu kama hicho, hilo ndilo jambo linalopendwa sana.

⁹⁷ Na imefikia mahali ambapo inaonekana kana kwamba hatujali wanawake wetu—au wanawake wetu hawajijali wenyewe. Hivyo ndivyo ilivyo. Mwanamke akiwa mwadilifu, mwanamume hana budi kuwa mwadilifu. Na hilo si kumuunga mkono mwanamume, lakini najua hilo ni kweli. Na ni kulingana na Maandiko. Biblia ilisema kuwa ingekuwa hivyo. Kwa hivyo tunaweza kuwa na ufufuo? Tunaweza kuwa na ufufuo?

⁹⁸ Sikiza, rafiki Mkristo. Katika muda mchache uliobaki hebu niwaulize jambo fulani. Tuna Billy Graham. Tuna Jack Shuler. Tuna aina zote mbali mbali za mienendo ya kidini inayoendelea ulimwenguni kote. Nao wamekuwa wakiendelea kwa miaka sita ama saba kote Marekani kwa nguvu kadiri wawezavyo kupiga hatua, na hamna mkutano wa ufufuo. Mbona? Milango inafungwa. Tumevua kila samaki, kama nilivyosema asubuhi hii, toka kidimbwini. Labda mmoja wawili wanajishikilia mahali fulani.

⁹⁹ Ambapo Billy Granham alikuwa na mkutano (naamini ilikuwa Boston au mahali fulani), nao walidai walipata waongofu elfu ishirini na kitu katika majuma sita. Walirudi kule majuma machache baadaye na hawangepata ishirini. Waza hilo! Ndugu, karibu tu imekwisha. Ningesema kitu fulani hapa. Ona?

¹⁰⁰ Tunaishi katika siku ambazo Mungu alinena zingekuwepo. Nasi tunaishi katika siku za mwisho. Nasi tunaishi katika wakati ambapo wanadamu... Haijalishi nini tunachojaribu kuwaza, Neno la Mungu lasema kuwa tumechaguliwa tangu asili. Naam. Na wale Mungu amewaita watamjia Mungu; na wale ambao Mungu hajawaita hawatamjia Mungu. Mungu huita, nao wakataa wito huo; wao hukataa... Sasa, sisemi Mungu humhukumu mtu ye yote. Yeye hapendi kwamba wote—kuwa ye yote apotee, bali wote wapate kutubu. Lakini ili awe Mungu, Yeye—Yeye alijua tangu mwanzo kwamba hawangukuja. Bali Yeye aliwapa nafasi, lakini hawangukuja.

¹⁰¹ Vipi... Kama Yeye hajui hilo, alijuaaje basi tungekuwa na magari yasiyo ya farasi? Angejuaaje wakati kama huu tulio nao sasa ungekuweko? Mbona Yeye alisema, “Wanadamu wangukuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa?” Mbona manabii wote wanatabiri kuwa mambo haya mengine yangetokea tangu mwanzo? Mungu alijua kila kitu. Yeye ajua yatakayokuwepo. Na kuna watu fulani ndani mle ambao Mungu aliwatazama katika wakati na kusema, “Hawatakuja.” Nao wamehukumiwa kwa hukumu huo, kwa sababu walichagua wenyewe. Amina! Naam.

¹⁰² Nami naamini, ndugu yangu, dada (Nasema hili kwa heshima ya Mungu na uchaji wa Mungu moyoni mwangu), naamini Amerika imezama! Imepotoka. Imekuwa duni kabisa hata ikainama chini. Msiba kweli huo.

¹⁰³ Waza tu hapa, kama ninavyosema katika—katika kujibu Maandiko haya, wanawake saba wangemshika mwanamume mmoja. Katika Vita Vya Kwanza vya Dunia—vile Vita vya Pili vya Dunia... nina kato nyumbani toka kwa gazeti. Ninyi wenyewe yasomeni. Kasema, “Imekuwa kwa uadilifu wa wanawake wetu Waamerika? Wawili kati ya watatu wa wanajeshi walioenda ng’ambo katika miezi sita ya kwanza walitalikiwa na wake zao.” Wawili kati ya watatu walitalikiwa.

Wanawake hawa waliondoka tu na kutoroka. Mbona hivyo? Kama mtaelewa, marafiki, ni roho ya wakati huu.

¹⁰⁴ Hatuna budi kuingia katika roho wa siku za mwisho wakati siku za mwisho zinapowadia. Nenda katika jumba la dansi, yakupasa uingie katika roho ya kucheza dansi, au hawatacheza dansi. Nenda kanisani, yakupasa uingie katika Roho ya kuabudu kabla hujaabudu. Ulimwengu hauna budi kuingia katika roho ya siku za mwisho kabla siku za mwisho hazijakuja, nasi tuko katika roho ya siku za mwisho. Na Mungu ameahidi kuwa mambo haya yangukuwa hapa, na hayo ndiyo tuliyo nayo. Sisi tuko katika siku za mwisho. Na wanaume na wanawake wangani wamelala na hawafahamu.

¹⁰⁵ Na uadilifu... Nilikutana na mvulana mdogo hapa hivi majuzi kule... ee, hivi punde, mwishoni mwa mwaka uliopita. Naye alikuwa akiniambia mimi, mvulana mdogo wa shule ya sekondari aliyekuwa ameo. Akasema, "Nilimwoa msichana huyu, kwa sababu alikuwa msichana mzuri, na ilinipasa nimwoe kabla hajamaliza shule ya sekondari." Kasema, "Hatuwapata kuwa na hata mmoja bikira, kwa kadiri nijuavyo, katika shule ya sekondari miaka mingi hapa." Ona? Ni watovu wa uadilifu sana.

¹⁰⁶ Na kule—California nilipitia katika njia za mji katika mahali ambapo polisi wangekwambia uondoke kwenye hizo njia. Kuna hatari zaidi kwa mwanamume kupitia kwenye njia za mji kuliko kwa mwanamke. Vichochoro vyenye giza. Ee, Mungu, uturehemu! Je, hamjui Biblia ilisema mambo hayo yangetimia?

¹⁰⁷ Na kabla tu Yeye hajatoa kivuli chake katika Sodom na Gomora, na kuenda chini pale, jambo lile lile lilitukia—lilitendeka, samahani. Kisha Mungu akawashushia moto na kupateketeza mahali pale. Ishara madhubuti kuonyesha kuwa ulimwengu umekwisha, ufikiapo mahali pale, ungepokea [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] kitu hicho.

¹⁰⁸ Tuko katika siku za mwisho. Bila shaka. Wanawake saba wangemshika mwanamume mmoja, wakisema, "Tutakula chakula chetu wenyewe na kuvaa mavazi yetu wenyewe, ila tu na tuitwe kwa jina lako kuondoa aibu yetu." Ndugu, haikupasi uondoke Marekani. Kuna mahali pamoja pekee ambapo nimeona maishani mwangu ambapo nilidhani palikuwa pabaya zaidi kuliko kwenye njia za mji na mambo ambayo nimeona katika taifa letu. Na hatuwi bora kwa vyo vyote vile. Tunazidi kuwa waovu na waovu zaidi wakati wote. Na kumbuka, ninanena katika Jina la Bwana. Tutaendelea kuwa waovu zaidi. Kuna tumaini moja pekee, nalo ni katika Kristo Yesu. Haijalishi utafanya nini.

¹⁰⁹ Nimepaza sauti, nimepitia taifani kote hapa. Na Mungu hata amefufua wafu. Nasi tulienda mijini; na watu wameamka ambao wamekuwa katika viti vya kusukumia wagonjwa kwa miaka

mingi, na kutembea kote mjini wakifuata magari, wakisukuma magari yao na kadhalika. Na wanawake, ama ambao madaktari wao wametangaza wamekufa, wakibeba picha za X-ray zilizo na jina la daktari juu yake, walifufuliwa toka kwa wafu. Na mji ule ulirudi nyuma na kusema, “Enhee, ni uwezo wa kushirikiana mawazo; kundi la watakatifu wanaojigaragaza.” Lo, huwezi kutarajia kingine ila laana! Ee! Vema!

¹¹⁰ Hukumu iko hapa; huna budi kuipata. Ndugu, ikimbie ghadhabu inayokuja na umwendee Kristo Yesu upesi uwezavyo! Ondokea mambo haya! Naam, ni roho ya siku za mwisho. Mambo mengi yangesemwa. Nitaharakisha.

18. Tafadhali, waweza kutwambia sisi Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kriso Kristo anavyotutarajia kuja katika nyumba ya Bwana wetu kuabudu?

¹¹¹ Vema, hilo ni nzuri. Hilo ni muhimu sana kwa kanisa lo lote. Mungu akutarajia wewe kuja kanisani... Sasa, hilo ni swali tu, swali lifaalo. Halina Maandiko; ni—bali linayo. Ngoja, nitawaambia yale Yeye alisema, kitu cha kwanza, ukitaka Andiko, watu wanapaswa kuja katika nyumba ya Mungu kwa kusudi moja, hilo ni kuabudu, kuimba nyimbo, na kumwabudu Mungu. Hivyo ndivyo Mungu anavyotarajia. Yeye hatutarajii sisi kuingia katika nyumba ya Mungu kuongea habari za—au cho chote kile, au kusengenyana, au kunena kuhusu yale tutakayofanya juma nzima; Yeye atutarajia sisi kuja kumwabudu. Ni nyumba ya kuabudia. “Na mambo yote yatendeke kwa uzuri na kwa taratibu,” kasema Paulo katika Biblia. Kila kitu kinapaswa kuwa sawa. Kunapaswa kuwe na ujumbe.

¹¹² Jambo la kwanza ambalo ningesema, kulingana na sheria za Kanisa katika Agano la Kale—au Agano Jipya samahani, kwanza, watu waliingia kwenye kanisa la—la Mungu katika Roho wa kuabudu. Nao walipoingia, nyimbo ziliimbwa. Na labda mhubiri angehubiri, kwa maana yeye alikuwa nabii wa kanisa. (Nabii wa Agano Jipya ni mhubiri; twajua hilo: “Ushuhuda wa Yesu Kristo ndio Roho ya unabii,” kasema Ufunuo.)

¹¹³ Sasa, mhubiri aanza kuhubiri. Alipokuwa akihubiri, baraka, tuseme labda mwishoni mwa mahubiri makuu, zikaanza kushuka; watu wangesema, “Amina,” kaanza kumhimidi Mungu. Ndipo mara tu alipomaliza kuhubiri, huenda ujumbe ukatokea, labda katika kunena kwa lugha zisizojulikana (1 Wakorintho 14:13, 14). Ndipo—ndipo kama hakuna mfasiri kanisani, mtu huyu apaswa kutulia, kwa sababu wananena kwa lugha sahihi, lakini wao wanafanya hivyo mbele za Mungu. Ona? Lakini kama wananena kwa lugha na kuna mfasiri, yule mfasiri anapaswa kutoa ujumbe huo. Makanisa yote yanafikia hapo.

¹¹⁴ Charles Fuller, kadiri tu alivyofanya fujo na kunipinga kuhusu hayo nilipokuwa kule, yeye anakubaliana nayo sasa. Nao wanafanya hayo kule kote katika Long Beach. Naam, bwana! Mumo humo—mumo humo kwenye ukumbi, akiwa na baraka za Mungu, akinena kwa lugha, kutafsiri kwa lugha, na kuwaombea wagonjwa. Naye alisimama uso kwa uso pamoja nami na kusema, “Ndugu Branham, siamini upuzi huo.”

Nilisema, “Vema, ni juu yako. Si kwa wasioamini, Ndugu Fuller, ni kwa hao wanaoamini.” Na sasa yeye anahubiri jambo lile lile. Inafikia wakati fulani. Kuna shindano la uamuzi.

¹¹⁵ Sasa basi, kama ni utaratibu, kama hili ndilo unalofikia . . . Mhubiri anaponena kila kitu chapaswa kutulia kumsikiza mhubiri. Maana hapo mna Neno la Mungu linaloendelea, kama yeye anahubiri chini ya upako. Ndipo kila roho ya manabii anatii manabii. Mchungaji ajapo jukwaani, afungue hiyo Biblia, kanisa linapaswa kunyamaza, likimsikiza anapofunua Maandiko, kusikiza yale atakayosema. Kama akisema neno linalokufurahisha waweza kusema, “Amina, Bwana asifiwe!” au lo lote utakalo. *Amina* maana yake ni “na iwe hivyo.” Biblia ilisema ufanye hilo.

¹¹⁶ Kisha, ujumbe unapokwisha . . . Ndipo mhubiri akitoa nafasi ndani mle ambapo watu wote wanafurahi, Roho kati ya watu, huenda akatuma ujumbe mwingine. Akituma ujumbe, utamjia mtu fulani, ndipo tafsiri yake haitakuwa ku—kunukuu-nukuu. Maandiko au kufanya jambo fulani. Mungu hapayuki-payuki. Lakini utakuwa ujumbe wa moja kwa moja kwamba mtu fulani atende jambo *fulani* au cho chote kile ambacho kitajenga kanisa. Ndipo Kanisa likijengeka, iwapo wao . . .

¹¹⁷ Kama kwa mfano hivi: Mtu fulani asimame hapa na kunena kwa lugha; huyu atafsiri na kusema, “ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI; *Fulani* akamwekelee mikono mtu huyu hapa, kwa maana ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI, usiku huu ndio wakati wa kuponywa kwake.” Ni nini?

Kisha mtu huyu huyu kasema, “Nilikuwa nimeketi pale; moyo wangu ulikuwa ukiwaka kwa ajili ya huyo mtoto mchanga.” Sasa—sasa wao wanaamka kwa kumtii Roho, waenda na kuweka mikono yao kwa huyo mtoto mchanga, akapona. Kama haikutendeka, kuna kasoro fulani. Ona ona, ona? Ni ujumbe moja kwa moja.

¹¹⁸ Kisha asiyeamini aketi pale na kusema, “Ngoja kidogo.” Kasema, “Mungu yu pamoja na watu hawa!” Mwaona lile ninalomaanisha?

¹¹⁹ Ndipo wao watasema—au, “ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI: Kila mtu, aliye upande wa kusini wa mji, toka kwa hiyo barabara iitwayo Spring na kuendelea, na ahame katika siku mbili zijazo, maana kunakuja kimbunga kitakachofagia sehemu

hiyo yote ya mji.” Ndipo, muda si muda, kuna unabii kwa kanisa lote.

¹²⁰ Kisha mtu fulani—aliye na upambanuzi wa kiroho—aamke na kusema, “Je, huo ulikuwa wa Bwana?” Kila mmoja. Kama watu wazuri watatu watasimama na kusema—upambanuzi wa kiroho—waseme, “Huo ulikuwa wa Bwana,” basi kanisa linaupokea; na kila mtu katika sehemu hiyo ya mji anahama, aondoka kule katika wakati huo. Ndipo usipotimia inawapasa kumshika mtu huyo. Mna roho mwingine miongoni mwenu. Lakini unapotimia, basi mhimidini Mungu na mumshukuru Mungu kwa kuwasalimisha katika ghadhabu iliyokuwa ikija. Ona? Chunguzeni mambo hayo. Hilo ni Kanisa katika utaratibu.

¹²¹ Jumbe mbili ama tatu—si zaidi ya tatu—zitatokea kwa wakati mmoja hivyo. Lo lote lililo nje, yapasa liwekwe katika utaratibu. Kwanza . . . kisha kanisa lingine, jambo lingine katika utaratibu . . .

¹²² Sijui. Huyu huenda akawa ni mwanamke aliyeuliza hili. Nili . . . Jambo lingine limeingia niani mwangu, kwa hivyo heri nilinene. Mwanamke, alipokuja kanisani, kulingana na Agano Jipya, alipaswa kuingia na kuketi mwenye uso uliotiwa utaji na wenye huzuni, na aketi hivyo ibada nzima. Hiyo ni kulingana na Maandiko. Naam. Lakini nadhani mwanamke . . . Bila shaka. Sasa, siwalaumu ninyi wanawake. Ona?

¹²³ Mwanamke kijana alinjia muda mchache uliopita. Si . . . Ndugu Junior alikuwepo pale huyo mwanamke aliponijia, kwamba alikuwa na shida fulani. Jirani zake walimcheka, kwa sababu hangekata nywele zake hapa muda mchache uliopita. Naye akaenda na kukata nywele zake. Ndiposa, mwanamke fulani ng’amboni mwa mtoni alimtatanisha, na kumwambia yeye angeondoa roho zake, afunge miguu yake kwa nywele—nywele zake, na akamfanya mwanamke huyu kuingiwa na fadhaa. Huyu Mwanamke karibu arukwe na akili zake—ana watoto wawili. Hakujua la kufanya. Alikuwa tu ameketi hivyo.

¹²⁴ Yeye akaja kwa motokaa akaisimamisha mbele ya nyumba siku moja. Roho Mtakatifu akashuka, akanena naye, na akamwambia kuwa yeye atapona, na “ROHO ASEMA HIVI. . .” Naye—naye alikaa hivyo wakati huo na kwa siku chache, kisha yeye . . . Nilienda jana, nilienda kumwona huyo mwanamke nikiwa pamoja na Ndugu Junior na Ndugu Funk. Nami nilikuwa umbali wa nusu maili. Yeye alikuwa amesimama, akichanua nywele zake ambazo ange-angeziachilia zikue sasa, kasema, “Acha majirani wacheke na wafanye cho chote watakacho.”

¹²⁵ Kisha Roho Mtakatifu hangeniruhusu niende kule. Naye akanena na kumwambia kuwa nilikuwa karibu na mahali pale kisha akataka kuja. Na usiku uliopita katika ono, nilimwona mwanamke yule akija, na nikamwambia kilichompata; naye aliponywa chumbani mwangu muda mchache uliopita. Ona?

Sivyo, Ndugu Junior? Naam. Muda mchache tu uliopita. Ona? Mungu hangeniruhusu niende kule kwa sababu kitu kile hakikuwa tayari bado. Ona? Yeye alinileta hapa hadi mahali fulani na kulithibitisha papo hapo, kuonyesha haikuwa mwanadamu, ilikuwa Mungu. Ona?

Basi, yeye alisema, “Ndugu Branham, mume wangu ananitaka niwe na nywele ndefu.”

¹²⁶ Nilisema, “Mungu ataka jambo lile lile.” Naam, kwa maana imewapasa wanawake kuwa na nywele ndefu. Hicho ndicho kifuniko chao.

¹²⁷ Najua mabibi hawa siku hizi—au ninyi mabibi, samahani, huvalia kofia. Mnasema hicho ndicho kifuniko chenu. Ni kosa. Biblia ilisema kifuniko cha mwanamke ni nywele zake. Naye akikata nywele zake ni jambo la kawaida yeye kuomba. Sivyo? Hayo ni Maandiko. Ona? Kwa hivyo sasa, wanawake wanapaswa kuwa na nywele ndefu, haijalishi unavyotaka kuwaza juu yake, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Nionyesheni mahali po pote. . .

¹²⁸ Unasema, “Vema, nywele zangu ni ndefu. Ona, zimefika mabegani. Hiyo ilikuwa nywele fupi. “Kristo. . .” Ulisema, “Kristo alikuwa na nywele ndefu.” La, Yeye hakuwa nazo kamwe. Kristo alikuwa na nywele zilizofika mabegani, ndivyo wasemavyo. Wao—wao wanaivuta tu hivi na kuikata, urefu wa mabegani. Tazama neno la Kiyunani kuhusu hilo ndani mle, na utaona.

¹²⁹ Nywele za kike. . . Mwanamume hapaswi kuwa na nywele ndefu, kwa sababu ni za kike, zinazofika humu. Lakini Yeye alilikata hapa mabegani Mwake, ambapo wao huikata, kuzunguka kichwa Chake, kuifupisha tu hivyo: Hiyo ilikuwa nywele fupi.

¹³⁰ Kwa hivyo, wanawake mlio na nywele zifikazo mabegani, bado ni nywele fupi. Sasa, sisemi hilo litawapeleka kuzimuni wala kuwapeleka Mbinguni. Hilo halifai kitu. Lakini taratibu ya Kanisa ni wanawake wawe na nywele ndefu. Naam; ndivyo. Na kuingia kanisani. . . Na—na asiwe na shughuli zo zote katika mambo, mambo ya umma—wala ku—nakusudia shughuli kanisani. Naye apaswa kuwa mtiifu, na mnyenyekevu, na kadhalika kwa sababu ndiye, Biblia ilisema, aliyesababisha kule kuanguka kwa kwanza. Naam; hiyo ni kweli. Sasa, upesi sana. Natumai hilo halikudhuru.

19. Swali: Mbona ono la Mungu lilinijia mimi nilipokuwa karibu kupokea Ushirika kanisani mwangu? Upande wa pill. (Vema, ni jina la mwanamke; naam, ni jina la mwanamke,) A. . . Mbona ono la Mungu lilinijia mimi nilipokuwa karibu kupokea Ushirika kanisani mwangu?

¹³¹ Vema, singejua, Dada, isipokuwa iwe hivi: Iwapo ulimwona Kristo akikutokea katika ono kanisani mwako ulipokuwa ukipokea Ushirika, Yeye alikuwa akikujulisha hili: ya kwamba

ulikuwa unampokea Yeye katika mfano. Ushirika unawakilisha ule mwili wa Yesu Kristo; nawe ulikuwa ukimpokea Yeye kama mfano katika mwili wako. Kwa hivyo ishi msafi, na ishi mwadilifu.

¹³² Sikiza. Ukipokea Ushirika (mtalisikia likisomwa katika dakika chache) isivyostahili, una hatia ya Damu na Mwili wa Yesu Kristo. Mtu na apokee Ushirika huo na aishi sahihi mbele za Mungu, apokeaye ushirika huo, samahani, aishi sahihi mbele za Mungu. Usipokee isivyostahili. Hilo tu ni . . .

¹³³ Tazama. Biblia ilitabiri katika siku za mwisho kuwa meza zote za Mungu zingejaa matapiko. Na hakungekuwa na ye yote awezaye ku—kufahamu. Sivyo? Tazama. Nilienda si muda mrefu uliopita katika maskani makuu. Sitataja jina lake; nyote mwayajua vizuri. Mwajua kile wanachotumia kwa Ushirika? Walipokea mkate, mkate mzima—mkate mwepesi, na wakaukata-kata. Na kundi la mashemasi, ambalo huyo mhubiri alisema saba kati yao ni walevi. . . Naam. Na kila mmoja wao, kundi lote. . . Ungewaona walipokuwa wakitembea jengoni mle wakiongea na watu. Na kanisa lilipokwisha, mwishoni, kati ya shule ya Jumapili na kanisa, karibu kila mmoja, mchungaji na wote hao, walienda nje na kuvuta sigara huko nje, na wakarudi ndani na kupokea Ushirika wa Bwana. Mungu alisema ya kwamba hatakuhesabia asiye na hatia kwa ajili yake. “Na wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamekufa.” Naam.

¹³⁴ Kasema, “Meza zote za Mungu zimejaa matapiko, nani atakayewafundisha mafundisho.” Yeye alisema, “Kwa maana kanuni haina budi kuwa juu ya kanuni, mstari juu ya mstari, na huku kidogo, na huku kidogo. Shikilia yaliyo mema. Maana kwa ndimi za kugugumiza na lugha nyingine nitanena na watu hawa, na hii ndiyo raha niliyosema ingekuja, lakini na hawa wote wangetikisa vichwa vyao wakaondoka na kusema, ‘Hatutayasikia.’” Tazama tunakoishi, marafiki. Ee, rehema! Amkeni!

¹³⁵ Naam, ono lako, Dada. . . Kama wewe u mtu mwema, msafi, mwanamke mtakatifu mbele za Mungu, ulikuwa umesimama pale na Yesu alikuwa akikujulisha ya kwamba Yeye alikuwa akitoa Ushirika, ambapo unampokea Yeye ndani mle kama mfano; na kama sivyo, ilikuwa onyo kwako kuwa sahihi mbele za Mungu kabla hujaupokea tena.

20. Ningetaka kujua maana—maana ya yafuatayo: I Timotheo, sura ya 2—II Timotheo sura ya 2 na kifungu cha 16.

¹³⁶ Hebu kidogo. 2 Timotheo. . . [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] . . mnakusanyika. Labda hamwezi kukubaliana na yale nilisema. Mtakapoenda nyumbani. . . Basi, nendeni nyumbani na kusoma kirefu sana, ndiposa hilo litawasaidieni kuwa wa kiroho. Vema, II Timotheo 2 na 16 inasomeka hivi:

Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya kidini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu,

**Naam! Pia, nataka kujua nini maana ya “yasiyo na maana.”
“Yasiyo na maana—jiepushe na maneno yasiyo na maana,
kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu.”**

¹³⁷ Sasa, jambo la kwanza ni “maneno yasiyo na maana kwa kuwa wataendelea.” Sasa, cho chote kilicho cha kale—kinaendelea tu kupayuka. Biblia ilisema—Yesu alisema, “Bali ‘ndiyo’ yetu iwe ‘ndiyo’ na ‘siyo’ yetu iwe ‘siyo’ kwa kuwa yazidiyo hayo yataleta dhambi.” Haiwapasi hata kufanya mizaha na kuchekeshana ninyi kwa ninyi. Mungu atakuhukumia kila neno lisilo maana unalonena. Mwajua hilo? Biblia ilisema kuwa itakupasa uhukumiwe kwa kila neno lisilo maana. Kwa hivyo yatupasa tuwe watu wa jinsi gani? Watu wanyofu, thabiti, wanaopendana, wakarimu, na wala si kundi la wapumbavu, kila mara kuendelea . . .

¹³⁸ Tazama. Mchukue mtu atakayeanza leo . . . Nimeng’amua hilo kwangu binafsi, na asili yangu binafsi, ni M-Irish; kila mara nina mizaha mingi, na vichekesho na yasiyofaa. Na kila—kila mara mke wangu husema, “Sasa, Bill . . . !”

Mimi husema, “Naam, Mpenzi.” Yeye atasema, nikicheza na watoto . . . Nasema . . . Kuwachekesha au kitu fulani, kasema, “Vema mwajua, kuna watu watatu mashuhuri waliotoka Kentucky.”

“Hao ni akina nani?”

“Vema, Abraham Lincoln.”

“Naam.”

“Daniel Boone.”

“Enhee.”

“Na baba yenu.” Kitu kama hicho.

¹³⁹ Naye angesema, “Sasa, Bill, umeanza mambo yako tena.” Nami yanipasa niende kwenye chumba cha siri mahali fulani na kusema, “Bwana, nisamehe, sikukusudia hilo. Nifanyie kitu fulani; nifanye niache hayo.” Ona?

¹⁴⁰ Na kila siku mimi—nikifanya hilo . . . Sasa, tulikuwa tukinena kuhusu neno *kuanguka* asubuhi hii. Unapofanya hivyo umekwisha kuanguka. Naam, bwana! Yakupasa utubu. Sivyo? Sasa, sikusudii kusema ulienda ulimwenguni nawe ulitenda *hiki* na *kile*, lakini umetenda jambo fulani. Yakupasa utubu na ufe kila siku ili uishi katika Yesu Kristo. Kwa hivyo kila siku—kila siku, yakupasa ufe kila siku upate kuishi katika Kristo Yesu.

¹⁴¹ Nionapo kitu fulani . . . Wakati mwingi mimi hufanya vitu ambavyo si halali. Nitakuwa nje, na mtu fulani atasema jambo fulani, huenda nikafanya mzaha kidogo kuhusu hilo. Mtu fulani aseme . . . Si mibaya; sasa, siamini Wakristo hunena mizaha

michafu. La, bwana! La, bwana! Hilo hata haliwapasi Wakristo, Biblia ilisema. Ilisema tuyakatae mambo yasiyo ya kidini kama hayo, na mizaha, na kucheza-cheza, na mengineyo kama hayo. La, Wakristo hawaneni mambo hayo; Wakristo wana nia safi.

¹⁴² Lakini usipochunga, mara kwa mara utapata mtu. . . Yeye atafanya mzaha mdogo leo. Vema basi, yeye alidhania kuwa ulikuwa halali, naye hataujali, hatawaza tena habari zake. Siku inayofuata atafanya mizaha miwili midogo. Ona? Ndipo muda si muda, unafanya jambo jingine. Kisha muda si muda, inakurudisha kwa ule mtindo wa kale tena? Sivyo? Achilia mbali mambo hayo. Jiepushe nayo! Pia jiepushe na maneno yasiyofaa.

¹⁴³ Acha mtu fulani aje. . . Nitawapa tu mfano mdogo. “Bi. Doe, wajua nini? Nilimwona mumeo. Hebu nikuambie. Uki. . .” Ona? Wakati. . .

Sasa, nadhani tu. . . Sema, “Sitaki kuyasikia!” Waondokee. Hatachukua zaidi ya hayo, nao watayakatiza. Naam.

¹⁴⁴ “Vema, wajua nini, Dada? Nitakwambia nini kilimpata Ndugu.” Si dada pekee, bali ndugu pia—Ona;

“Ndugu, nitakwambia kilichotendeka. Unajua kama tungemwondoa mhubiri huyu, kama tungefanya *hili*, au kumwondoa huyu shemasi, au tufanye *hivi*.” Jamani! Ji—ji—jiepushe na kitu kile.

¹⁴⁵ Nafikiri kitu kizuri unachopaswa kuweka juu ya dawati lako ni kitu kidogo nilichoona kule Florida muda mchache uliopita. Ilikuwa tumbili wadogo watatu; moja wao alikuwa amefunika macho yake kwa mikono, na kusema, “Usitazame maovu,” na mwingine alitia vidole vyake maskioni mwake, kasema “Usisikie maovu!” na mwingine alifunika kinywa chake kwa mkono wake, akisema, “Usinene maovu.” Nadhani hilo lilikuwa jambo zuri, sivyo? Naam, bwana! Ee, lo! Hilo ni jambo nzuri sana.

¹⁴⁶ Weka mawazo yako safi na kwa Kristo. Unadhani unasema sasa. . . Sasa ona, usipochunga, utajikuta mwenyewe mahali fulani, ukiendelea kuwaza hilo. . . Wewe Usi—usiwaze hilo. . . Huwezi kuishi mkamilifu sana hata usifanye kosa hilo sasa. Naam, usidhani utakuwa hivyo, kwa sababu hutakuwa. La, bwana! Wewe si asiyetenda dhambi, na utaenda kando ya njia, upande huu au upande ule.

¹⁴⁷ Lakini mtu aliyeangushwa chini mara moja, kama yeye yu askari ataamka tena. “Bwana, hebu niamke na nijaribu tena.” Lakini mwoga, mara tu aonapo anaanza kufanya kosa lake ndogo la kwanza, yeye ni kama nilivyosema asubuhi hii, mdudu na buibui wa majini na atatambaa moja kwa moja hadi majini tena. Ona? Yeye hawezi kustahimili.

¹⁴⁸ Kwa hivyo kataa maneno yote ya kale—ambayo hayafaidi na endelea, kunena. *Kupayuka* maana yake ni “mchafuko.” Na Biblia ilisema “Waangalieni wale wafanyao fitina kati yenu.”

¹⁴⁹ Kama mtu fulani asema, “Enhee! Enhee,” sasa—sasa hebu sema, “Washindaje? Nina furaha kukuona tena. Asante.” Na aendelea tu. Hilo ndilo jambo bora. Usijiepushe nao, bali waangalie tu. Usiwasikize, kwa sababu waona yanakoelekea.

21. Yesu alikuwa wapi tangu—Yesu alikuwa wapi tangu ubatizo Wake hata ile miaka mitatu ya huduma Yake?

¹⁵⁰ Vema. Yesu, Yeye alipobatizwa, alitoka moja kwa moja majini, na Roho alimwongoza kwa siku arobaini mchana na usiku ajaribiwe na ibilisi. Naye akajaribiwa kwa siku arobaini mchana na usiku. Akafunga. Akatoka. Shetani alimjaribu alipomaliza kule kufunga Kwake. Na Yeye alimshinda ibilisi kwa Neno la Mungu, na kuingia katika huduma Yake, na kuhubiri kwa miaka mitatu na nusu, kulingana na Maandiko.

¹⁵¹ Tazama. Nyuma kule katika Danieli, Mungu alinena na kusema Yeye angehubiri kwa miaka mitatu na nusu na akatiliwe mbali kwa sadaka wakati huo. Ndivyo hasa. Yeye aliamriwa kabla msingi wa ulimwengu. Naam.

¹⁵² Mathayo sura ya 4, mtapata hayo. Kama hailingani hasa na imani yenu, sawa.

Sasa, hilo mimi . . . Hebu tuone vile . . . Ee, naam! Aliamriwa hapo awali. Tuna hilo, sivyo . . . ? . . .

22. Wakati mmoja—wakati mmoja sisi sote tulikuwa weupe ama weusi? Kati ya hawa wawili, yupi alilaaniwa?

¹⁵³ Sasa, kwa kadiri tujuavyo, singewaambia kama Adamu na Hawa wa—walikuwa weupe, au kahawia, au manjano, au weusi. Siwezi kuwaambia. Hapana ajuaye ila Mungu pekee, nadhani: Ndiye alikuwepo nyuma kule. Sasa, katika . . . Kama tulivyotoka sisi sote kwa lugha moja na watu wamoja hadi ule mnara wa Babeli, mchafuko. Ndiposa lugha zao zikawa tofauti. Na kwa kadiri tujuavyo watu wote walikuwa watu wamoja hadi wakati huo. Nao waligawanyika na kutawanyika katika sehemu mbalimbali za ulimwengu.

¹⁵⁴ Na baadhi . . . Mchukue mnyama; uchukue kiumbe cho chote kinachokula aina fulani ya mchanga, kitageuka rangi hiyo. Mimi—kama mna mwindaji hapa, unifuata tu kwa dakika chache. Enda chini kule Mexico ukamchukue mbwa mwitu; kuja hapa katika Arizona ukamchukue mbwa mwitu; enda Kaskazini ukamchukue mbwa mwitu yule yule, na tazama zile rangi tatu. Mchukue mbwa mwitu yule yule, na tazama zile rangi tatu. Mchukue mjuzi mkubwa ajabu aliyekuzwa Texas, na umchukue aliyekuzwa Arizona na uone tofauti kati yao (Ona?), kwa sababu ni udongo wanamoishi. Ona?

¹⁵⁵ Na sasa, yule Msiami—Msiami ni mtu wa ma—manjano, Wajapani, na kadhalika, na Msiami. Mkushi ni m—mtu mweusi, au Mnegro tulio nao sasa. Naye alienda kule katika nchi hizo za giza chini kule.

¹⁵⁶ Nao—na—nao wa...Ndiposa watu weupe walikuwa Wa-Anglo-Saxon ambao ni sisi. Na—au watu hapa, wale tuwaitao watu weupe, walitoka Uingereza ambayo hapo awali iliitwa “Nchi ya Malaika.” Na kwa sababu wao walikuwa weupe, na wenye nywele za shaba, na kadhalika...Na wakatawanyika Ireland, na Norway, na kwingineko—mle. Nao wote walitoka kwa Wa-Anglo-Saxon.

¹⁵⁷ Sasa, gani walikuwa wa kwanza, na ni akina nani waliolaaniwa? Si hata mmoja wao. Najua kile unachojaribu kufikia. Unajaribu kumfikia Hamu. Najua unakoenda—kwa watu wa Hamu.

¹⁵⁸ Sasa, kulikuwa na Hamu, Shemu, na Yafethi. Sasa Hamu, yeye—yeye—yeye hakujaribu kuufunika uchi wa baba yake, lakini alimcheke na kumfanyia mzaha. Na Mungu alimlaani Hamu kwa kuutazama uchi wa baba yake na kutokujaribu kufunika aibu yake. Na Shemu na Yafethi walisaidia na kutanda mavazi yao juu ya baba yao alipokuwa amelala uchi. Na sasa, Mungu alimwambia Hamu kuwa uzao wake ungewatumikia wengine.

¹⁵⁹ Sasa, kama ulidhani hiyo ni laana juu ya weusi, vema basi, Wayahudi nao pia ni weusi. Kama unadhani hilo lingekuwa kile—kile—kile tukiitacho mtu mweusi au Wanegro wa nchi hii walioko humu sasa, yakupasa uende kule India. Wahindi ni weusi sana kuliko Wanegro. Nimekuwa katika nchi hizo zote mbili. Hawa hapa wale—wale wakushi chini kule Ethiopia, na Waafrika, mtu mweusi tumjuaye siku hizi. Wako chini, kule, wengi wao bado wa zamani za kwanza—katika makabila yao. Kama tu tulivyokuwa Yesu alipokuja.

¹⁶⁰ Watu weupe walikuwa tu wa zamani za kwanza kama wale—wale wenyeji wa Afrika walivyo sasa, labda wa kikale zaidi. Kumbuka miaka elfu mbili iliyopita tulikuwa watu wa makabila uchi nje kule pamoja na—na upinde na mishale na shoka za mawe za kuwindia (naam hasa), sisi watu Wa-Anglo-Saxon. Ndivyo hasa. Kwa hivyo yupi alikuwa yupi?

¹⁶¹ Nitawaambia siku hizi wale waliolaaniwa ni wale waliomkataa Yesu Kristo. Hivyo tu. Wale wampokeao Yesu Kristo wamebarikiwa.

¹⁶² Sasa, huwezi kusema...Nitaenda kule, niwachukue Waeskimo, toka kwa nchi hiyo kule. Na ndiye huyo kule, na mtu huyo ni mweusi kuliko watu weusi tulio nao hapa. Naenda kule India na kuwaona hao Wahidi; na yeye ni—yeye si mtu aliyechanganyika rangi, yeye ni—yeye ni mtu mweusi. Yeye ni mweusi kuliko—wa rangi nyeusi kabisa. Naye ndiye aitwaye... Na ni Mhindi. Vema sasa, katika Afrika twawakuta baadhi ya watu wa Afrika ambao ni...Wengine wao si weusi sana; wengine wao karibu ni kama weupe; na wengine wao ni—ni tofauti.

163 Nenda kwa Wayahudi; na—unasema Wayahudi wana sura nyeusi. Wayahudi ni watu wa rangi ya kahawia, lakini nimewaona wengine wenye nywele nyekundu na macho ya samawati, ngozi ya kadiri. Ona?

164 Kwa hivyo jambo lote ni hili: sisi sote tulitoka kwa ukoo mmoja. Naam. Nasi sote tulilaaniwa katika kule kuanguka kwa Hawa. Nasi sote tunaokolewa kwa kufufuka kwa Yesu Kristo. Ndivyo mambo yalivyo. Kwa hivyo hakuna laana. Waliolaaniwa ni wale wasioamini, lakini waliobarikiwa ni wale wanaoaminio. Kwa hivyo hakuna ye yote, marafiki, mtu mweusi au chotara, au mtu mweupe au mtu manjano. Wao... Kama mtu mweusi alilaaniwa kwa kuwa mweusi, basi mtu manjano amelaaniwa nusu. Ndiposa wale—ndiposa mtu wa manjano—halafu mtu wa kahawia, yeye amelaaniwa theluthi mbili. Ona, ona? Na ndipo Waafrika wamelaaniwa karibu nne kwa tano. Nami nadhani Wahindi wamelaaniwa kabisa basi. Loo, masalale! upuzi vipi! La! Ni mazingara tofauti na kadhalika watu wanamoishi. Waligeuka kuwa weusi na kadhalika...?...

165 Watazame Wahindi wa Amerika. Wengi wao...Wale Wanavajo kule ni watu wa ukoo mweusi kuliko watu weusi wa Kushi katika nchi hii, wale Wanavajo. Waapaches ni... Wao wana rangi—ya—ya shaba nyekundu. Na makabila mbali mbali...Ona? Kwa hivyo papo hapo kati ya Wahindi, papa hapa, unawakuta weusi, na karibu...Na wale Wacherokee karibu wana rangi nyeupe kama tulivyo sisi, wale Wacherokee. Na papa hapa kuna katika taifa hili, makabila mbalimbali. Kwa hivyo mwaona, huwezi kusema wamelaaniwa nusu na wamelaaniwa kabisa. Hawakulaaniwa kwa sababu eti wao ni weusi. Hawalaaniwi kwa sababu wao ni manjano au kwa sababu wao ni weupe. Kunayo tu laana moja niijuayo, na hiyo ni kutokumwamini Yesu Kristo. (Najua, Danny, ni wakati wangu wa kumaliza, lakini ninayo maswali mawili zaidi.)

23. Vema sasa. Yako wapi yale makabila ya Israeli kumi yaliyotawanyika na kupotea (Mwanzo 44:49), lile kabila la Yusufo kwa mataifa mengi? Simeoni, Lawi, ambao hawakuwa na nchi yao wenyewe, lakini walitawanyika kati ya yale makabila mengine kumi... Yako wapi yale makabila kumi? Je, twaweza kupata walipo?

166 Naam, bwana! Yanaweza kupatikana yalipo. Kigeografia yanaweza kutambuliwa yalipo katika Biblia. Na Mungu atwambia pale watakapokuwa katika siku za mwisho na mwisho wao utakuwaje. Na sasa hivi, ndiyo kwanza nisome kitabu ambacho...?...Israeli ambapo wale wengine walikuwa. Wao walisema kuwa mmoja alichovya miguu yake katika mafuta na kadhalika. Mungu ajua walipo, wanaishi mahali mbalimbali. Na Wayahudi wote wanarudi Palestina, ambako Mungu aliahidi katika siku za mwisho wangukuwa kule.

24. Swali moja Zaidi: **Naweza—siwezi kuamini kuwa Mungu alituma vita kama hukumu. Siwezi kuamini kuwa Mungu hutuma vita kama hukumu.** (Hebu sikizeni tu kwa muda mchache.) **Siamini, kama wengine wafanyavyo, kuwa Mungu aweka upanga katika mikono ya hawa wachinjaji tangu Babeli ya kale hata kwa Hitler, kuwaua wanawake na watoto wasio na hatia—pamoja na wenye hatia, waitekeleze hukumu ya Mungu. Na Mungu—Mungu wangu wa upendo hangefanya—Mungu wangu wa upendo (Kunradhi!)—hangefanya hili. Vita ni kazi ya Shetani. Tafadhali thibitisha farakano hili.**

¹⁶⁷ Sasa, hebu kidogo. Nililisoma hili muda mchache uliopita, ndiyo sababu nikaliweka mwisho. Sasa nawatakeni ninyi mtulie kwa kitambo kidogo. Sasa, hebu—hebu tupate hili moja kwa moja, kwa sababu hili ni swali nzito. Na lazima liendewe kwa unyenyekevu. Mara tu baada ya hilo, kama mwaweza tu kutustahimili kidogo tena . . .

¹⁶⁸ Najua kunachelewa lakini ni . . . Kumbukeni, na hilo je? Sasa, waweza kuenda kucheza dansi usiku mzima na usiwaze lo lote kulihusu (ona?), kukaa kwa vitu vya kilimwengu, lakini ifikiapo Neno la Mungu kupitisha dakika ishirini, ndugu, yatupasa tupate mhubiri mpya. Ona? Ni aibu. Paulo alihubiri usiku kucha. Nilihubiri hapa miaka mingi iliyopita hadi saa 8 na 9 usiku. Na watu walitembea juu na chini mahali hapa waki—wakimsifu Mungu saa 8 au saa 9 usiku. Ungeliwaona yapata watu dazan moja huku wakimpokea Roho Mtakatifu saa 8 na saa 9 usiku. Mungu uturehemu. Laiti ningeliziona tena. Lakini hatuwezi; siku hizo zimepita. Siku hizo hazimo tena; wakati umeendelea sana, sasa. Usiku umekaribia na watu wana . . . “Vema, hatujali tena, kwa hivyo . . . Lo . . . ? . . . jitayarishe kuingia.” Na hivyo tu—hivyo tu ndivyo iendavyo.

¹⁶⁹ Ngoja, nataka kukuuliza jambo fulani sasa. Sasa, sitakubaliana nawe, Ndugu ama Dada, sijui. Liliwekwa humu asubuhi hii. Nilikuwa nalo katika Biblia yangu na nilikuwa nikilitazama muda mchache uliopita. Sasa, kwa njia ya kirafiki . . . Na sasa, sitaki u—u—unirukie. Nataka unisikize kwa makini.

¹⁷⁰ Basi kumbuka, ningalipenda tu kukubaliana nawe kwa hili—kwa uamuzi wako kuhusu hili kama nilivyofanya kwa huyo mwanamke, maskini mwanamke yule muda mchache uliopita. Kasema . . . Yeye na mume wake, walitoroka tu na kuoana; hivyo tu. Lakini yeye ameweka nadhiri; yakupasa uishikilie. Ona? Na sasa, yanipasa nikae na Neno la Mungu.

¹⁷¹ Lakini sasa “Siamini . . .” Lakini kwanza, “Siwezi kuamini kuwa Mungu hutuma vita kama hukumu.” Vema, sasa, rafiki, kama kuna jambo moja pekee lisilo sawa kwa imani yako, na hilo ni, si la Kimaandiko. Mungu hutuma vita kama hukumu. Naam.

Mimi—mimi nitakupa Maandiko; sitalisoma hapa tu ndiposa nikwambie.

¹⁷² Tazama. “Siamini kama wafanyavyo wengine kuwa Mungu aliweka upanga katika mikono ya hawa wachinjaji tangu Babeli ya kale hata kwa Hitler, awaue wanawake na watoto wasio na hatia.” Kama ningelikwambia katika Jina la Yesu Kristo kuwa Yeye alifanya hilo, na ningelithibitisha kwa Biblia, je ungeliamini basi (ona?), kuwa Yeye alilifanya, au—na Yeye atalifanya tena? Vema. Sikiza hili.

¹⁷³ Sijui. Huenda huyu akawa rafiki msiri wangu anayeketi hapa nijuavyo; maana Mungu aliye Mbinguni ajua siujui mwandiko huu. Singeliwaambia. Lakini nawatakeni msikize hili. “Mungu wangu ni Mungu wa upendo—Mungu wangu ni upendo na hangelifanya hili. Vita ni vya Shetani.” Nitakubaliana nawe kuwa vita ni vya Shetani. Ndivyo hasa. Yeye ndiye mtawala wa ulimwengu huu. Kila falme na kila taifa ulimwenguni humu ni vya Shetani. Mungu alisema hivyo katika Neno Lake. Shetani alisema, “Hivyo ni vyangu.” Yesu alikubali kuwa vilikuwa vyake. Lakini Yeye atakuwa mrithi wake hatimaye, Yesu atavirithi. Hatutakuwa tena na vita wakati huo. Lakini Mungu huruhusu Shetani afanye hili kwa ajili ya masahihisho na kwa hukumu.

¹⁷⁴ Sasa, nataka kukuuliza jambo fulani kabla hatujaanza. Nataka unijibu mimi hili upate kujua. Kama huamini kuwa Mungu ni... (ulisema)... hangetenda mambo haya. Kuanzia tu toka mwanzoni... Sasa, nisikizeni kwa makini sana mkiweza. Sikiza. Mbona Mungu Mwenyewe alimrudi Mwanawe na kumuulia msalabani? Mungu alimuua Mwanawe msalabani. “Bali ilimpendeza Mungu,” yasema Maandiko, “kumpiga sana Yeye, na kumchabua, na kumjeruhi Yeye.” Mungu alimfanyia hivyo Mwanawe kuniokoa mimi.

¹⁷⁵ Nataka kukuuliza kuhusu Sauli, yule mfalme mkuu wa Israeli. Mungu alimwambia yeye ashuke aende akamteke nyara Mfalme Ogi na kila kitu alichokuwa nacho na akaangamize kila kitu chini pale, wanaume, wanawake, watoto na kila kitu... Na Sauli... hata awaue ng’ombe, kisisalie cho chote hai. Na Sauli alienda chini kule na akabakiza ng’ombe kadha. Naye Mungu akaondoa Roho toka kwake na akamtenga Naye; yeye akawa adui wa Mungu.

¹⁷⁶ Mbona Eliya alisimama pale Mungu alipomtia maskini Mfalme Ogi mi—mikononi mwa Ahabu? Naye alimwambia Ahabu amwue mfalme huyo. Na Ahabu alikataa kufanya hilo. Na Eliya nabii alikuwa na msaidizi aliyesema, “Nipige kwa upanga wako,” mlisoma habari zake... Yeye alikuwa nabii.

Yeye alisema, “Siwezi.” Naye akapoteza uhai wake. Ndipo yeye akamwambia mwingine, kasema, “Nipige.” Na mtu yule akampiga kwa upanga na kumkata. Naye alijifunga mwenyewe

kwa mavazi ya utani na akasimama pale. Na hapa akaja Ahabu akiendesha gari lake.

Yeye alisema, “Mbona—mbona umesimama hapa?”

Yeye alisema, “Vema, nilikuwa mlinzi, niliamriwa kumlinda mtu. Na yeye alinipiga mimi na kutoroka,” Yeye alisema, “nami nikamwachilia aende. Nao waliniambia kama ningefanya hivyo, itanilazimu kulipa kwa maisha yangu.”

Yeye alisema, “Vema, utalipa kwa maisha yako mwenyewe.”

Yeye alijifunua na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, kwa maana hukumwua mfalme huyo kule, utalipia kwa nafsi yako mwenyewe.” Naam? Hilo ni sawa hasa.

¹⁷⁷ Hebu niwasomee kitu fulani hapa. Vipi kuhusu Babeli, Yoshua alipo—Mungu alipomtuma Yoshua kule, naye aliangamiza kabisa watoto wachanga, watoto, na kila kitu, na hakuacha hata kitu kimoja hai. Yeye aliangamiza kila kitu. Watoto wachanga Wafilisti, yeye aliwaangamiza, tu. Mungu alimwamuru. Na kama yeye hakufanya hilo, ilikuwa maisha yake mwenyewe.

¹⁷⁸ Nitakunyosha sasa hivi. Mungu ni upendo, upendo mkamilifu; lakini hujui upendo ni nini. Hiyo ndiyo sababu siku hizi watu hawajui imani ni nini. Mungu ni upendo. Yampasa Yeye awe katika upendo; Yeye ana mamlaka yote juu ya Neno Lake. Na Yeye apaswa kutimiza Neno Lake. Yeye yampasa akupende. Na kama anakupenda, hana budi kukulinda.

¹⁷⁹ Sikiliza hapa. Mnanena kuhusu kuangamizwa kwa watoto. Hebu kidogo, hebu niwaonyeshe kitu fulani hapa Maandikoni, yale—yale Biblia isemayo kuhusu mambo haya hapa. Hebu twende hapa tusikize tu haya kwa dakika moja na kuona yale Mungu alisema. Sasa, ninasoma toka Ezeieli sura ya 9, mkitaka kuiandika. Sikizeni kwa makini.

Kisha... akilia kwa sauti kuu masikioni mwangu, akisema, waamuru wale wanaousimamia mji wakaribie, ... kila moja na awe na kitu chake cha kuangamizia mikononi mwake. (Sasa, huyu ni Mungu akinena.)

Na tazama, watu sita wakaja, wakitokea kwa njia ya lango la juu, lielekealo mkononi mwake; na mtu mmoja kati yao amevaa bafta, naye ana kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. Wakaingia, wakisimama karibu—karibu na madhahabu ya shaba.

Na huo utukufu wa Bwana wa Israeli ulikuwa umepanda juu kutoka kwa kerubi, ambaye ulikuwa juu yake, mpaka kizingiti cha nyumba; akaniita—mtu yule aliyekuwa amevaa bafta, mwenye kidau—aliyekuwa na... kidau cha wino cha mwandishi mkononi—ama kiunoni;

Na kwa hivyo... Na BWANA... (Herufi kubwa B-W-A-N-A, ambaye ni Mungu.)... BWANA akamwambia, pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, ... ukatie alama katika vipaji vya nyuso vya watu wanaougua na... kulia kwa sababu ya... machukizo yote... yanayofanyika kati yake.

Na hao wengine... (BWANA)... aliwaambia, nami nalisikia, pitieni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiache, wala msione huruma; (Tazama, kifungu cha 6.)

Kabisa—waueni kabisa mzee, ... na kijana, ... wanawali... na watoto wachanga, na... wanawake, ... (Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo!)... lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika kiingilio—katika patakatifu—Basi, wakaanza kwa wazee... waliokuwa mbele ya nyumba.

¹⁸⁰ Kwa maneno mengine, Mungu aliwaambia watu hawa, “Sasa, ngojeni; nitawatia alama watu kwanza, wale waliojitolea kwa Mungu kabisa...” Akawatia alama. Yeye akawaambia, “Sasa, kwa watu hawa walio na silaha za kuangamia, ninyi pitieni kati na msiwaonee huruma wanawake, watoto wala cho chote, lakini angamizeni kabisa kila kitu.”

¹⁸¹ Katika ule ulimwengu kabla ya gharika katika maangamizi wakati mamilioni mara mamilioni na mabilioni ya watu yalikuwa juu uso wa ya nchi, na Mungu akamtuma mhubiri mzee wa utakatifu aliyetwa Nuhu, na kuhubiri kwa miaka mia na ishirini, na kuwaambia waingie katika safina, na hao ambao hawakuvingia safinani wangeangamia... Na Mwenyezi Mungu, aliyekuwa na mamlaka juu ya mbingu, alishusha mvua iliyoangamiza kabisa mamilioni ya wazee, ya vijana, watoto wachanga, wakitetemeka na kuangamia majini.

¹⁸² Mwenyezi Mungu—na Yeye hakika ni Mungu wa upendo. Na hilo ni kweli. Yampasa awe. Yeye awapenda walio Wake. Yeye yampasa awe na mamlaka yote juu ya Neno Lake. Kwa hivyo si kwa—kwa mabishano, lakini sikubaliani nawe. Mungu wako wa upendo...

¹⁸³ Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa nikizungumza... Labda ni Shahidi wa Yehova. Mtu huyo alikuja na kuniambia, “Ndugu Branham, je, wakusudia kuniambia kuwa unaamini kuna kuzimu kunakowaka moto?”

Nilisema, “Si yale nisemayo, ni yale Biblia isemayo.”

Yeye alisema, “Je, unataka kuniambia kuwa Baba mwenye upendo wa mbinguni angewateketeza watoto Wake? Naam,” kasema, “wewe hungeteketeza mtoto wako.”

Nilisema, “La, bwana!”

“Vema basi, kama wewe mwanadamu una upendo kama huo (ona, jinsi watu wawezavyo kuvuruga-vuruga kitu kile?)—kama wewe mwanadamu una upendo mwingi vile, wadhani Baba wa mbinguni atupendaye angewaangamiza watoto Wake?”

¹⁸⁴ Nilisema, “Hasha!” Yeye haangamizi watoto Wake, lakini wewe u mtoto wa nani? Mungu haangamizi watoto Wake, Yeye anajaribu awezavyo kuwaingiza ndani. Lakini ni ibilisi aliyeachiliwa atakayewaangamiza watoto wake. Kwa hivyo Mungu humruhusu tu Ibilisi.

¹⁸⁵ Tazama. Nani aliyeruhusu uovu ushuke na shetani aende kuangamiza mtumishi aliyekuwa mkamilifu sana wa Mungu hata kufikia wakati wa Yesu Kristo, watoto wake na kila kitu yeye alichokuwa nacho—Ayubu? Na Mungu alituma pepo mchafu kule na kuangamiza watoto wote wa Ayubu na kila kitu kumjaribu tu mtumishi Wake. Sivyo? Hakika.

¹⁸⁶ Lo, ningesimama hapa kwa saa nzima na kuwaonyesha hayo—Ndugu yangu, Dada. Naam, ye yote uliye. Usimtatanishe huyu Roho wa Mungu. Vita ni hukumu ya Mungu juu ya mataifa. Maangamizi hutumwa na Mungu. Biblia ilisema hivyo.

Na Mungu ni Mungu wa upendo, lakini Mungu ni Mungu wa hasira pia. Nawe hutasimaa mbele ya . . . Hilo limekuwa jambo linalodhuru kanisa siku hizi.

¹⁸⁷ “Baba atupendaye, bila shaka Yeye hatajali nikitenda hiki.” Ukitaka kufanya hilo, heri uende ukalifanye, kwa sababu kwanza upendo wa Mungu haumo ndani yako.

¹⁸⁸ Tunajitayarisha kupokea Ushirika katika muda mchache, nami nataka hili likolee kabisa. Jambo ni kwamba, kilicho moyoni mwako kitazaa—kitafanya maisha yako. Aina ya mbegu uliyoweka ardhini itazaa kwa jinsi yake. Wawezaje kuchukua mmea wa m—mhindi na u—uvune gugu kwake? Huwezi kufanya hivyo zaidi ya unavyoweza kugeuza punje ya mahindi na ikawa kwekwe. Hungeweza kufanya hayo, kwa sababu yana asili mbili tofauti, maisha mawili kwa jumla. Wa—wa—waweza kuchukua mbegu ya gugu na mbegu ya kitunguu, na zinaonekana sawasawa kabisa hata mtu bora sana hangezitenganisha. Naam. Jambo pekee likupasalo kufanya ni kuzipanda. Zote mbili zaonekana sawa kwa umbo lakini zipande. Zote zitazaa, na moja itakuwa gugu na nyingine itakuwa kitunguu. Hiyo ni kweli hasa.

¹⁸⁹ Aisee, “Mbona—nini kifanyacho mbegu hii—inafanana sana na hii—itoe uhai tofauti?” Ni kwa sababu uhai aina hiyo umo ndani yake.

¹⁹⁰ Na mwanamume au mwanamke anayekiri kuwa Mkristo na haishi maisha kama hayo, kwa neema ya Mungu, ni gugu. Kwa matunda yao mtawajua. Kama kitu kile ki moyoni mwako, chashuhudia jinsi ulivyo mahali fulani pengine. Kama ni mbovu, inashuhudia kuwa wewe uko hivyo chini hapa. Unapokufa, utaenda tu ambako tayari uko.

Kama wewe u mzuri na u—u mzuri kwa sababu Mungu amekufanya mzuri, na umezaliwa mara ya pili, huna budi kuelekea hivyo, kwa sababu Uhai huo utapaswa kushuhudia pamoja na mahali hapa. Kama unashuhudia hapa, hapo ndipo utakapokwenda. Kama unashuhudia juu kule, huko ndiko utakakokwenda.

¹⁹¹ Jinsi ulivyo, wewe... Shika hili mawazoni mwako sasa. Nitamaliza. Lakini jinsi ulivyo hapa ni ishara kuwa wewe u kitu fulani kinginecho mahali fulani. Daima mmetaka kuwa katika ukamilifu, ninyi Wakristo. Kuna ukamilifu, na ukamilifu huo haumo katika maisha haya. Lakini kila mwanamume na mwanamke hapa aliye Mkristo, kila mtu aliye Mkristo hapa sasa amekwisha tukuzwa katika uwepo wa Yesu Kristo. Na una mwili mwingine. Hautakuwa nao wakati mwingine, unao hivi sasa. Hivi sasa kuna mwili mwingine unaokungoja wewe kama huu ukiangamia. Je, ungewaza hilo. Chunguza hilo kidogo.

¹⁹² Je, wajua kila mmoja wetu aweza kuwa utukufuni kabla mapambazuko kesho asubuhi? Sasa, kama wewe si Mkristo, rafiki yangu, kuna jambo moja tu lililobaki kwako. Huna budi kushika hiyo njia. Kama uko njiani, huna budi kuendea njia hiyo. Kama wewe u punje la mhindi, utazaa mahindi. Kama u kwekwe, utazaa uhai wa kwekwe. Sasa, kama umekuwa—u wa kanisa mahali fulani ambalo halijui na halifundishi, na linakuacha tu wewe uje kanisani na uwe mshiriki wa kanisa... Unasema, “Vema, Ndugu Branham, kanisa langu hufundisha kuwa yatupasa tumpokee Yesu Kristo kama Mwokozi wetu binafsi. Kama tunamwamini Bwana yesu Kristo tumeokoka.” Kama maisha yako hayalingani na hilo, hujafaulu bado.

¹⁹³ Je, mwajua ibilisi anaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu? Je, mwajua Yesu hadharani—je, mwajua ibilisi alimkiri Yesu hadharani kuwa Mwana wa Mungu? Na yeye hakuokolewa. Na hangeokolewa; yeye ni ibilisi. Kwa hivyo kumkiri Yesu kuwa Mwana wa Mungu...

¹⁹⁴ Je, mwajua hao Mafarisayo na Masadukayo wote, kila mmoja alikuwa msafi kabisa na watu wa kidini; jinsi walivyompenda Mungu kwa mioyo yao yote, nia zao; na wakashindwa kumwona Yule asiye na hatia, Mwana wa Mungu, kumtambua kuwa Mwana wa Mungu. Walakini, walikuwa wa kidini sana (sivyo?) wacha Mungu sana, wanavyuoni kweli kweli, walijua Biblia vema kuliko ye yote wa wanavyooni wetu wa siku hizi. Hawakuwa na kazi yo yote ila kuketi pale vizazi vyao vyote na kumtumikia Bwana.

¹⁹⁵ Sasa, tazama yale Maandiko husema: “Katika siku za mwisho...” Kweni, rafiki zangu Wakristo, na kwa upendo wa kiungu, Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho watu—ingefikia wakati ambapo wangukuwa wakaidi, wenye kujivuna,

wanaopenda anasa kuliko wanavyompenda Mungu.” Sasa, si hayo ni kweli?

¹⁹⁶ Mtu fulani katika jengo hili alienda kwenye karamu ya Mwaka mpya hivi majuzi, na katika ukumbi walikuwa na vinywaji baridi na tamasha na wakiendelea kufanya yasiyofaa, chakula cha jioni chenye mtindi wa maziwa, na kadhalika. Makanisa hata yanaandaa dansi. Yale hasa Mungu aliyowaambia wasifanye, wayafanya katika Jina la Kristo. Na haya ndiyo Yesu aliambia Kanisa litende, nao wanayakana. Yesu—haya ndiyo maneno Yake ya mwisho, mapenzi Yake na agano kwa Kanisa: “Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumwa. (Labda huo ndio umbali mchungaji aliosoma. Lakini mengine yaliyobaki ndiyo haya). Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika nyoka au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

¹⁹⁷ Sasa, haya ndiyo Yesu alisema watende katika Jina Lake. Wao hukana kuwa hili lipo, lakini wao huenda na kutenda kinyume cha yale Yeye alisema, kufundisha kuwa hayo yamepita, hamna kitu kwayo, na kufundisha theologia badala yake. Lo, si ajabu tuko katika bali tuliyomo.

¹⁹⁸ Tazama hapa, hebu nikwambie, Ndugu yangu. Kanisa lifikapo mahali ambapo ki—kila mshiriki ndani mle amejazwa sana na Roho Mtakatifu pamoja na nguvu, hata hizo ishara zinafuatana. . .

¹⁹⁹ Nawaza kuhusu Mtakatifu Paulo nje kule kwenye kisiwa kile baada ya kuvunjikiwa jahazi. Mungu alimpa ono. Wakati zile siku kumi na nne mchana na usiku. . . Matumaini yote yalikwisha isha ya kwamba wangeokolewa kamwe. Maskini jahazi hilo ndogo lilikuwa likichukuliwa huku na huko hivyo, nao wote walikuwa wakilia, siku kumi na nne mchana na usiku. Paulo alikuwa chini kule, akaona ono. Akatoka nje, naye akasema, “Jipeni moyo, kwa kuwa Malaika wa Bwana, ambaye mimi ni mtumishi Wake amesimama karibu nami, akaniambia, ‘Usiogope, huna budi kusimama mbele ya Kaisari. Tena, tazama, Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe.’”

²⁰⁰ Jahazi hilo lilipovunjika nao wakaifikia pwani, wakachanganyikana kule na wenyeji, Paulo alikuwa akiokota kuni, naye akaenda na kuziweka motoni. Na ndani mle kulikuwa na nyoka mkubwa, akamzonga-zonga mkononi. Sasa, huyo nyoka aliingiza sumu ambayo—mkononi mwake ambayo ingalimuua haipati dakika moja. Wale wenyeji walisema, “Tazama mtu huyo akianguka na kufa, kwa kuwa yeye atakufa kwa ghafla. Yeye amekuwa wazimu kwa kuhubiri Injili.”

201 Watu wa kidini walimfunga kwa minyororo. Mekanisa bora sana yaliyokuwepo siku hizo yalimfunga minyororo. Kama si kwa ajili ya Katiba ya Marekani, mngeona jambo lile lile siku hizi. Hiyo ni kweli! Ngoja tu hadi—itakapoharibika zaidi kidogo.

202 Na nyoka akamzonga-zonga ghafla mkononi. Sasa tazama. Paulo hakuogopa. Yeye alisema, “Yesu Kristo alisema, ‘wakishika nyoka, hawatawadhuru.’” Kwa hivyo akasogea humu, akamtukusia motoni; akageuka na kuenda kuleta kuni zingine na kuziweka tena motoni; akageuka na kupasha moto mgongo, na akageuka tena kuipasha mikono yake. Wale wenyeji wakaulizana, “Mbona yeye hafi? Mbona mtu huyo hafi? Mbona yeye haanguki chini kwa kufa ghafla?” Lakini Paulo alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu (ona lile ninalomaanisha?), amejawa sana na Roho Mtakatifu hata sumu ile haingemfisha.

203 Ee, ndugu, nipe kanisa lililojaa Roho Mtakatifu. Mungu atatenda kwa mwaka mmoja ambayo wanatheologia wote wameshindwa kufanya katika miaka elfu mbili. Ngoja hadi ule upako wa Kanisa utakaposhika kabisa. Wana imani, lile kundi ndogo lililosalia. Baada ya milango ya Mataifa kufungwa, tazama, Mungu atapaka Kanisa wakati huo. “Mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu. Na mwenye haki na azidi kufanya haki, na yeye aliye mtakatifu na azidi kutakaswa.” Na Mungu atapaka Kanisa Nguvu za Mungu, na mambo yatatendeka. Si wakati huo pekee, lakini Yeye anafanya hivyo sasa.

204 Tazama ishara na maajabu; ndipo watu wanatazama hapa na pale na kusema, “Vema, ni ya ibilisi.” Lo, kwa sababu hawajui Maandiko, wala nguvu za Mungu. Na hiyo ndiyo sababu liko pale.

205 Bwana na awabariki. Nasikitika kwa kuwachelewesha hivi. Ni mara chache mimi hutenda hili, lakini sikutani nanyi sana. Huenda sikuyajibu maswali haya kulingana na mawazo yenu na kadhalika. Hayo yalikuwa yale mawili yaliyojibiwa asubihi hii. Kama sikufanya hivyo, Mungu awabariki. Nami si—sikukusudia ku—au kuwaudhi ninyi au cho chote kile. Ilinipasa tu niseme yale. . . Mliniuliza mimi maswali. Nikawapa ninyi majibu vizuri ni juavyo. Hiyo ni kweli.

206 Sasa, sijui mengi zaidi kuhusu vitu labda. Sijui lo lote nipaswalo kujua. Lakini jambo moja nijualo, Yesu Kristo hutuokoa sisi toka dhambini, hutukinga na dhambi, na hutupa sisi nguvu Zake na baraka Zake.

207 Na ukitazama hapa na pale na kuona yale yanayotendeka kwa watu wanaoombewa. . . Tazama kote mataifani na tazama ishara na maajabu kila mahali. Na tazama wakati unaokuja. Tazama hayo matawi mawili tuliyohubiri hapa wakati fulani uliopita, tukaanzia Mwanzo, jinsi yanatoa ushuhuda wao kila mahali. Jinsi yule asiyeamini, wa kiasili sana na mashuhuri

katika dini yake, lakini wana namna ya utauwa, bali wakikana nguvu zake. . . Na Kanisa linasonga mbele.

²⁰⁸ Na Bwana Yesu ambariki kila mmoja ndilo ombi langu. Na muishi mkiwa na mzigo sana—na Mungu aweke juu yenu watu—mzigo mzito kwa nafsi zilizopotea hata huwezi kulala mchana na usiku. Na Mungu ayajalie haya Maskani ya Branham majaliwa ya kuwa na mzigo sana hivyo. Sijali kama hampigi shangwe, au hamfanyi kingine cho chote, mradi tu mmelemewa na mzigo sana kwa nafsi zilizopotea hata hamwezi kulala. Mtakapofanya hilo, ulimwengu utakuwa ukijipenyeza humu pole pole uombewe (naam!), ulimwengu ukija kuombewa, mtajulikana kila mahali. Mungu na atupe sisi Roho Wake, atufanye wanyenyekevu, atuvunje-vunje, na kutufanya tujawe na nguvu za Mungu kuponya wagonjwa, kutoa pepo, kufanya ishara kuu na maajabu. Unapoweka mikono yako juu ya wagonjwa na kuomba baraka hiyo bila wimbi moja moyoni mwako, unaamini kuwa Mungu atayatenda. Tazama mahali hapo na pataanza kupata nafuu. Kwa nini? Mwovu ametuondokea. Kama tu mti uliokuwa umesimama, Yesu akautazama, na hakukuwa na tunda juu yake. Yeye alisema, “Na ulaaniwe.”

Masaa ishirini na manne baadaye wakapitia hapo. Petro akasema, “Tazama, majani yamekwisha nyauka.” Kitu fulani kilikuwa kimetendeka. Neno la Mungu liliisha nenwa.

²⁰⁹ Yesu alisema, “Mwamini Mungu. Kwa maana ukivambia mlima huu ung’oke, na usione shaka, utakutii.” Amini Mungu.

Sasa, ni wakati wa Ushirika. Huku tumeinamisha vichwa vyetu nitamuuliza mtu fulani awafariji. . . ? . . .

²¹⁰ Bwana, hii ndiyo saa, wakati ambao labda wanaume na wanawake, Bwana, ulimwenguni kote wataona hiyo saa kuu ya hukumu ikikaribia wakati Mungu atahukumu mataifa yote katika msimamo wao wa kisiasa. Kila mahali, mahali pote, na kila mtu hana budi kusimama kwenye hukumu ya Mungu. Na Baba, tuna furaha sana kujua kuwa kuna kimbilio kwa watu hawa ambao—ambao wangependa kulikimbilia. Na njia hiyo ni kupitia kwa Yesu Kristo, ambaye ni—Mzao wa Daudi. Na twakushukuru Wewe, Baba mpendwa, kwa kumtuma Yeye duniani, kwamba Yeye alikuwa Njia ambayo tungepitia; Yeye angetuomba sisi, na kuondoa dhambi zetu, tupate kuikimbia hasira na hukumu ya Mungu. Twajua kuwa ghadhabu ile inakuja. Na Kama—kama Yohana alivyosema katika siku zilizopita, “Kimbieni hasira itakayokuja.”

²¹¹ Sasa, Bwana, twaomba tunapopokea Ushirika usiku huu kuwa utatutakasa sisi, Bwana, na Damu Yako ituoshayo; na kila dhambi ya watu hawa iondolewe. Naomba kwa unyenyekevu na kwa moyo mweupe, Mungu, kuwa hutamwacha mmoja wetu aupokee isivyostahili. Kwa maana Wewe umesema katika Neno Lako, tukifanya hivyo, sisi tuna hatia ya Mwili na Damu ya

Bwana. Sasa, Baba, fanya watu hawa watakatifu na waliowekwa wakfu, ili sisi tuupokee huu bila lawama.

²¹² Na sasa, Baba, twatambua Ushirika ulitolewa kwanza kule Misri. Na watu wale waliopokea Ushirika, mwana-kondoo na mkate, waliposhika safari, kwa miaka arobaini wao walisafiri jangwani; na hakukuwa na hata mmoja mdhaifu kati yao walipotoka jangwani. Wao walikuwa wamepokea Ushirika.

²¹³ Mungu turehemu. Naomba kuwa wagonjwa wote wataponywa, waliopotea wote wataokoka. Na wale walio wa kidehuri na wasiojali, na wasonge karibu na moto wa Mungu, wakipasha moto nafsi zao. Tujalie, Bwana. Tusamehe sisi na utusaidie. Twaomba katika Jina La Mwanao.

²¹⁴ Hali vichwa vimeinama, nashangaa (hali ndugu akitupa sauti ya wimbo kwa kinanda) kama kunaye mtu humu ambaye angeinua mkono wake na kusema, “Ndugu Bill, mimi—mimi kwa unyofu...kwa ajili ya hali na nafsi. Ni—ni—ninataka unikumbuke. Ni—ni—ninataka kupokea Roho Mtakatifu.” Je, waweza kuinua mkono wako...?...Mungu akubariki. Mungu akubariki wewe, na wewe, na wewe, wewe, na wewe. Mungu akubariki wewe, na wewe, Mungu akubariki, Bibi, wewe, na wewe, wewe, Ndugu. Lo, mikono kila mahali. Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki—Mungu akubariki, Dada—wewe, Dada, nauona mkono wako. Unataka kupokea Roho Mtakatifu—Mungu akubariki, Ndugu.

²¹⁵ Je, hautaki kutembea karibu zaidi. Kumbukeni marafiki, sisi tunaishi karibu na kule kuja kwa Bwana wetu. Sasa, Mungu anathibitisha Neno Lake, ishara na maajabu kila mahali.

²¹⁶ Sasa, hakika—Mungu hakuniruhusu niende kule nje na nitiwe mafuta na Roho Mtakatifu kutenda ishara na maajabu, nikarudi na kuhubiri Neno, na kadhalika, na kulibariki kila mahali, na kusikia mambo haya, isipokuwa Yeye anipe ufahamu fulani wa Neno Lake. Yeye hangeliruhusu hilo. Kwa hivyo najua yale ninayonena.

²¹⁷ Na kama wewe huna Yesu Kristo, bila Roho Mtakatifu, hebu Mungu asikuruhusu ustarehe kamwe hadi umepokea Roho Mtakatifu. Usidanganyike. Usichukue kamwe mojawapo wa haya maungamo ya macho makavu ya kidehuri na useme kuwa una Roho Mtakatifu. Humpokei Roho Mtakatifu unapoamini. Huamini upate kumpokea Roho Mtakatifu. Ni kipawa cha Mungu. Paulo alisema “Je, mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Kwa hivyo aminini. Na Mungu awapeni ninyi.

²¹⁸ Sasa, Baba, kwa wale walioinua mikono yao, naomba kuwa utawapa wao Utu wa Roho Mtakatifu hivi sasa. Na aje kindani katika wote hawa—mikono kumi au kumi na mitano iliyoynuliwa. Naomba kuwa utampa kila mmoja wao ubatizo wa Utu Wako. Nao wajazwe sana na Roho Mtakatifu, hata ishara na maajabu zitendeke maishani mwao, wataona aina zote za

ishara. Kama Yesu alivyosema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Tujalie, Baba. Twaomba kwa unyenyekevu katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Amina.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org